# Nipashe

Jumamosi Aprili 25, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580215

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

...rdian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



TOLEO MAALUMU

## Uzoefu wa uhasibu ulimsaidia Dk. Mengi ujasiriamali, uwekezaji stadi

UKURASA 3




UKURASA 11

# 37 wapona corona, 71 wasubiri vipimo

• **Zanzibar** yatangaza ongezeko wagonjwa wapya 15, wafanyakazi elimu ya juu wataka mambo 6, Polisi yaendelea uchunguzi wanaodaiwa kutoroka Amana... *Ukurasa 2,4*



**BAA LA CORONA**

**Nini maana ya karantini? Ni kujifungia kushiriki au kujitenga na watu ambao sio wagonjwa lakini wanaoweza kuwa walikutana na watu wenye virusi vya Corona. Lengo ni kuzuia kusambaa kwa ugonjwa kipindi dalili zinapojitokeza. WHO**

- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**

## DC ahamishia shuleni familia zilizopata mafuriko

UKURASA 4



Baadhi ya mafundi wa kushona wa Shirika la kuleta Maendeleo Vijijini (RDO-Mdabulo) kupitia vyuo vya ufundi stadi (VTC) vya shirika hilo, wilayani Mufindi, mkoani Iringa, wakishona barakoa ambazo ni rafiki na mazingira zinazofuliwa na kutumika tena, kama sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali katika kuzuia maambukizi ya virusi vya corona. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store

## Habari njema wanafunzi vyuo vikuu ujenzi hosteli

UKURASA 4

MICHEZO CHIRWA AFUNGWA AZAM FC UK.23 | MAONI, KATUNI UK.6

# Ofisa elimu mbaroni madai ya kumhonga ofisa Takukuru

**Na Dotto Mwaibale,** SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), inawashikilia Ofisa Elimu Vifaa na Takwimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba mkoani hapa, Albert Ngimba, na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Isenengwa wilayani humo, George Mmembwa, kwa tuhuma za kushawishi na kutoa hongo ya Sh. 500,000 kwa ofisa uchunguzi wa taasisi hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kwenye ofisi za Takukuru mkoani hapa, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Singida, Adili Elinipenda, alidai lengo la watuhumiwa hao kutenda kosa hilo ni kumshawishi ofisa huyo wa Takukuru awasaidie kwenye uchunguzi unaohusiana na tuhuma za ufujaji na ubadhirifu wa fedha zilizotolewa na serikali.

Alidai kuwa watuhumiwa kwa pamoja walishiriki katika ufujaji wa fedha hizo zilizotolewa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya nyumba za walimu na vyoo.

"Watuhumiwa hawa walikamatwa juzi majira ya saa nne usiku nyumbani kwa ofisa huyo wa Takukuru wakiwa wamempelekea kiasi hicho cha pesa ikiwa ni sehemu ya Sh. milioni nne walizokuwa wamemwahidi," alisema.

Kiongozi huyo wa Takukuru alisema uchunguzi wa tuhuma hizo bado unaendelea na utakapokamilika, watuhumiwa wote wawili watafikishwa mahakamani kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2007.

"Takukuru inatoa wito kwa wananchi kuongeza kasi ya ushirikiano kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa, pia kujitokeza mahakamani pindi wanapohitajika kutoa ushahidi wao," aliomba.

Elinipenda pia alibainisha kuwa katika kipindi cha Januari hadi Aprili mwaka huu, Takukuru mkoani hapa imewapandisha kizimbani watuhumiwa 13 wanaokabiliwa na tuhuma mbalimbali za vitendo vya rushwa. "Kuna kesi sita zenye jumla ya watuhumiwa 13 zilifikishwa mahakamani na kufunguliwa mashauri ya jinai, na kati ya kesi hizo, tatu zilitolewa hukumu na kushinda.

"Vilevile, katika kipindi husika, Takukuru mkoani hapa ilifanya operesheni maalum ya kufuatilia vyama vya ushirika, kupitia zoezi hili jumla ya fedha kiasi cha zaidi ya Sh. milioni 48.907) ziliokolewa," alisema.



Wakazi wa Kipunguni na vitongoji vyake wakipita katika daraja la Matembele lililojaa maji baada ya mvua kubwa kunyesha jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# 37 wapona corona, 71 wasubiri vipimo

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema wagonjwa 37 waliokuwa wamepata virusi vya corona, wamepona na kuruhusiwa kurejea nyumbani baada ya vipimo vya mwisho kuthibitisha hawana maambukizo.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliyesema hayo jana jijini Dar es Salaam na kubainisha kuwa wengine 71 kwa sasa wanasubiri vipimo vya mwisho.

"Wagonjwa hao 37 ni kati ya watu 108 waliothibitika kuwa na maambukizo ya virusi vya corona, lakini sasa hawana dalili zozote za ugonjwa kama homa, mafua na kikohozi," alisema.

Ummy alisema watu hao 108 hawana dalili zozote za ugonjwa kama vile homa au mwili kuchoka, lakini wako katika vituo vya matibabu kusubiri vipimo vya mwisho ili kuthibika kwamba hawana virusi vya corona kabla ya kuruhusiwa kutoka vituoni. Aliwataka watu waliopona ugonjwa huo kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya ili kujikinga na maambukizo mapya ya corona. "Upo utafiti uliofanyika nchi mbalimbali ikiwamo China, umeonyesha kuwa watu wanaweza kupata maambukizo mapya kama asilimia 14. Tunapenda kuwahimiza watu waliopona, watoe elimu ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona kwa jamii," aliagiza.

Waziri huyo aliwashukuru watumishi wa afya kwa kuendelea kutoa huduma kwa watu wenye maambukizo ya corona na kuwataka waendelee kuzitoa kwa watu wote wanaohitaji huduma za matibabu wakiwamo wenye dalili za ugonjwa huo.

"Tumeona kumeanza tabia ambayo ni kinyume cha taratibu za afya, hatutakiwi kuwakataa wagonjwa wenye dalili za maambukizo ya virusi vya corona.

"Nasisitiza kwamba watumishi wa afya wanakumbushwa kutekeleza wajibu wao kwa kuzingatia Mwongozo wa Taifa wa Kudhibiti Maambukizo wa Juni 2018, pamoja na Mwongozo wa Menejimenti ya Matibabu ya Ugonjwa wa COVID-19 wa Januari 2020 ili kujikinga na maambukizo wakati wa utoaji wa huduma kwa wagonjwa," aliagiza.

Ummy aliishukuru Kampuni ya Azam Group kwa msaada wa sabuni 300 na fedha Sh. milioni 50 kwa ajili ya mapambano dhidi ya ugonjwa huo. Alisema msaada huo utatumika kwa chakula cha wagonjwa na usafi kwenye vituo vya tiba vya Temeke, Amana na Kisoka-Mloganzila.

Visiwani Zanzibar, Wizara ya Afya jana ilitoa taarifa ya ongezeko la wagonjwa wapya 15 wa corona hivyo kufikia idadi ya wagonjwa 98 kutoka 83 waliotolewa taarifa Aprili 22. Kati yao, 10 ni wa Unguja na watano wanaishi Pemba.

# Wafanyakazi elimu ya juu wataka mambo 6 corona

**Na Augusta Njoji,** DODOMA MJINI

CHAMA cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu za Juu Tanzania(THTU), kimetoa mapendekezo sita ya namna ya kukabiliana na athari zinazotokana na janga la corona hususan kwenye sekta ya elimu.

Miongoni mwa mapendekezo hayo ni vyuo vikuu, taasisi za elimu ya juu na vyuo vya kati kutumia fursa za Tehama kuendelea na masomo yanayowezekana kwa njia ya mtandao ili kusaidia kupangilia vizuri mihula ya masomo.

Pia, kinapendekeza serikali irasimishe utaratibu wa utoaji wa elimu kupitia mitandao na vyombo vya habari ikiwamo redio na televisheni hasa wakati huu wa corona.

Akitoa mapendekezo hayo mbele ya waandishi wa habari jijini hapa jana, Mwenyekiti wa THTU Taifa, Dk. Paul Loisulie, alisema ugonjwa wa corona umeleta athari katika sekta ya elimu na wanaona ni wakati sasa kwa vyuo na taasisi hizo kunusuru hali hiyo badala ya kusubiri hadi ugonjwa huo uishe.

Alisema pamoja na jitihada za kudhibiti na kutokomeza ugonjwa huo, tayari athari zimeshaonekana na nyingine zitaonekana siku zijazo.

"Hatupaswi kuendelea kusimama katika taratibu za kawaida tulizozoea wakati corona imeshavuruga taratibu, ni lazima tujipange na kutafuta utaratibu mbadala wa kukabiliana na athari za sasa na zijazo," alisema.

Alisema THTU inashauri vyuo vionyeshe umahiri wao wa kutumia fursa za Tehama kuhakikisha vipindi vinaendelea kwa yale masomo yanayowezekana kwa njia ya mtandao.

"Hii ni njia mbadala ambayo itasaidia taasisi hizi kupangilia vizuri mihula ya masomo pale ugonjwa huu utakapodhibitiwa na kukaa kusubiri tatizo liishe ndipo kuchukua hatua ni kutojitendea haki wenyewe, kutoitendea haki jamii na nchi kwa ujumla," alisema.

Alitoa wito kwa serikali kuwezesha taasisi hizo kufanikisha malengo hayo na kutoa msaada kwa taasisi za binafsi ambazo kwa wakati huu zinapitia wakati mgumu kufuatia vyanzo vyao vikubwa vya mapato kusimama kutokana na wanafunzi wengi kutolipa ada kwa wakati huu.

Dk. Loisulie alisema utaratibu ulioanzishwa na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) wa utoaji wa elimu mtandaoni na kwenye televisheni, uboreshwe zaidi kwa kuhusisha redio ili kuwafikia wanafunzi wote nchi nzima.

"Ili kutoharibu mtiririko wa mihula, wanaweza wakatafutwa walimu wa kila somo na kurekodi vipindi (mada zote) ambazo zitarushwa kwenye redio zote nchi nzima na wanafunzi kutakiwa kusikiliza na kufanya majaribio," alisema.

Mwenyekiti huyo alishauri kampuni za simu zilizopo nchini kutafuta namna ya kupunguza gharama za vifurushi vyao vya intaneti na pia miamala yao wakati huu wa corona ili watu wengi wafanye malipo kwa kutumia mitandao ya simu bila kuhofia gharama.

"Fedha ambayo huwa inatumika kutimiza azma ya wajibu kwa jamii inaweza kusaidia kutumika kwa njia hii ya kupunguza gharama za miamala na vifurushi," alishauri.

Dk. Loisulie pia alishauri wizara zote zijielekeze katika kutengeneza taratibu na mazingira wezeshi yatakayoendelea kulinda mazingira ya kiuchumi na kijamii kwa mwananchi wa kawaida na pia kulinda shughuli za kiuchumi za biashara mbalimbali ili kulinda ajira za wafanyakazi wengi.

Pamoja na hayo, Mwenyekiti huyo alisema taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu zinapaswa kuchukua hatua ya kufanya utafiti na machapisho juu ya ugonjwa huo badala ya kusubiri machapisho na utafiti kutoka vyuo vya Ulaya na Marekani.

Pia, alisema ni wakati mwafaka wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa kutekeleza dhana ya Tanzania ya viwanda kwa kutengeneza bidhaa zitakazouzwa ndani na nje ya nchi ili kuondoa upungufu wa bidhaa na huduma zilizokuwa zinaletwa kutoka nje ya Tanzania kabla ya janga hilo.



TOLEO MAALUM

## DK. REGINALD ABRAHAM MENGI

"Sijawahi kufikiria kuwa umaskini ni tatizo, bali nachukulia kama changamoto. Umaskini haujawahi kunirudisha nyuma; bali unanipeleka mbele."

# Uzoefu wa uhasibu ulimsaidia ujasiriamali, uwekezaji stadi

**Na Nimi Mweta**

KATIKA kitabu kuhusu maisha yake, Dk. Reginald Abraham Mengi aliweka mkazo katika dhamira ya kufikia malengo, au kuweka malengo yanayofikika na kuweka bidii kuyafikia bila kusikiliza sauti za kumkatisha mtu tamaa. Wako wengi wanaoweka malengo kama hayo ila wakwame njiani, na sababu ziko nyingi, ikiwamo mabadiliko ya mazingira ambako malengo hayo yaliwekwa na matazamio ya kuyafikia. Eneo jingine ni kama aliyeweka malengo hayo amepitia njia ya kitaaluma na uzoefu kiutendaji kuzuia kuingia katika shimo ambalo mwingine aliyeiva zaidi angelikwepa. Labda hapo ndiyo kulikuwa na tofauti kati ya Dk. Mengi na wengine.

Moja ya vianzio muhimu vya kukwama kwa biashara hata zingekuwa na mawazo mazuri kiasi gani ni udhaifu wa kutawala fedha, na jinsi miradi au kiwango cha uwekezaji kinapoongezeka, ndiyo utawala fedha unahitaji kujichimbia katika taaluma. Endapo mhusika hana taaluma hiyo inakuwa vigumu kujua wasimamizi fedha wakiboronga au kufanya hujuma, hali ambayo siyo rahisi kutokea kwa mwekezaji au mjasiriamali mwenye uzoefu wa usimamizi fedha, yaani uhasibu. Ni nyenzo muhimu iliyomwezesha Dk. Mengi kutawala kampuni zake, si aendeshwe.

Ingekuwa suala ni hilo peke yake labda kungekuwa na watu wengi tu (siyo kadhaa au wachache kama inavyoelekea hapa nchini) wenye uwezo wa kusimamia biashara, kutawala fedha na kuzuia uharibifu katika miradi au kampuni wanazounda. Kuna eneo jingine ambalo zaidi limeshikwa na wageni au wawekezaji wenye uzoefu kifamilia na siyo miongoni mwa waliokuwa watawala katika kampuni binafsi au mashirika ya umma, kuacha serikalini, wa kipindi (au kizazi) cha Dk. Mengi. Ni kujua mbivu na mbichi kwa usimamizi wa fedha serikalini, mashirika ya umma.

Alikuwa mshirika (partner) wa kampuni ya uhasibu na ushauri (hasa katika masuala ya kodi, ambayo yanajumuisha masuala mengi ya kulinda mtaji, kupata faida na kutekeleza majukumu kwa wana hisa (au mwenye mali) na pia kulipa kodi kama jukumu nguli za ziada. Kampuni za wahasibu washauri mara nyingi zinajulikana kama za washauri kwa mambo ya kodi, jambo ambalo linawachanganya wasiojua au kubobea taaluma hiyo, hivyo kuchukua muda mrefu kupata tafsiri yake. Ila ukisikiliza kinachosemwa kwa mfano katika hotuba za Bajeti ya Serikali unakuta kuwa kuna uhusiano kati ya kulipa kodi na viwango vya mtaji, uzalishaji na faida halisi.

Kwa jumla mbobezi masuala ya kodi anatakiwa apate njia ya kuunganisha maeneo hayo matatu kupata mwelekeo wa kutimiza majukumu ya kampuni yanayoendana na matazamio ya huyo anayewekeza, washirika kama wapo, waajiriwa, na yaendane na viwango vilivyowekwa vya kodi kwa biashara kama hiyo. Ushauri kodi kwa maana hiyo ni kama ukaguzi wa ufanisi, ambako 'mafiga matatu' lazima yasimame ili kampuni iende, kwani moja likiteleza hakuna kinachoendа. Lazima malengo ya uwekezaji yafikiwe kwa maana ya kutopata hasara na ikiwezekana kuwe na faida ya kuridhisha, wafanyakazi walipwe na wafurahie kazi yao, na halafu serikali ipate mapato.



Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi (katikati), akifafanua jambo kwa Waziri Mkuu Frederick Sumaye, alipotembelea Banda la IPP katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa, Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam. Kulia ni Kapteni John Chiligati. **NA MPIGAPICHA WETU**

> Katu hakuna uwiano kati ya maslahi ya mwajiriwa na maslahi ya kampuni, kwani inabidi apate naye chochote anachoweza, awekeze kwake awe na kitu endelevu cha kumhakikishia mapato uzeeni.



Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, akiwa na moja ya tuzo alizowahi kuzipata katika shughuli zake za biashara.

Kipindi ambacho Dk.Mengi alianza kazi ya uhasibu hadi kuondoka kuingia katika uwekezaji, huku akiwa amepewa majukunmu ya ziada kama kusimamia viwango na mitihani ya uhasibu nchini kama mwenyekiti NBAA (bodi ya wahasibu na wakaguzi) ni kielelezo tosha cha yale aliyojifunza. Katika miaka ya 60 alikuwa Uingereza akisoma uhasibu hadi kiwango cha 'Chartered Accountant' yaani kuwa na hati kamilifu ya kufanya uhasibu kokote na aliingia rasmi sekta binafsi kama mjasiriamali, mwekezaji.

Ukiwasikiliza wasimamizi wa mashirika ya umma ambayo yalifikia kilele chake miaka ya 1970 na kuanza kulegalega au kuzorota kabisa miaka ya 1980, na kuuzwa kwa kupigwa mnada au kufilisiwa miaka ya 1990, unapata picha ya tatizo lililokuwapo. Ni nadra kusikia watendaji wa zamani wa mashirika hayo, au wanasiasa wenye 'kupenda chongo na kuita kengeza' wakieleza nini hasa lilikuwa tatizo katika fani hiyo ya mashirika ya umma. Utasikia hisia kuwa yalikwama au kufa wakati ilipopitishwa sera ya kubinafsisha, wakati hali halisi ni kwamba yalikwama na kulazimisha serikali kuyabinafsisha au kupiga mnada, penginepo kuyafilisi tu, kwani hayatibiki.

Dk Mengi alijifunza umuhimu wa mfumo wa umiliki katika kuendesha biashara kuwa hata makampuni yangekuwa mengi kiasi, inatosha kuwa kuna jicho la kuangalia maamuzi ya siku hadi siku katika kampuni yote ile, siyo kusimamia kila kitu. Pale ambapo mwenye mali (katika mashirika ya umma ni serikali yenyewe) akitegemea mwajiriwa (msimamizi wa shughuli) ndiye amwambie nini kinafanyika na nini kinahitajika, ni wazi kuwa shughuli hiyo itaporomoka. Katu hakuna uwiano kati ya maslahi ya mwajiriwa na maslahi ya kampuni, kwani inabidi apate naye chochote anachoweza, awekeze kwake awe na kitu endelevu cha kumhakikishia mapato uzeeni.

Ni eneo ambalo hakuliandikia au kulizungumzia sana kwani angewavuruga mawazo watu wengi lakini alisahihisha makosa aliyoyaona alipounda shughuli zake mwenyewe za ujasiriamali na uwekezaji, na hakuwahi kukwama, kufilisika, kampuni kuzorota, n.k. Alipanda kutoka hatua moja kwenda nyingine kwani alijua jinsi ya kuoanisha uwekezaji na mazingira, kwa kupunguza gharama pale mazingira yanapokuwa mabovu kwa matazamio ya tija (uwiano kati ya gharama za uwekezaji, uzalishaji na mauzo, mapato na faida, kabla ya kuitafakari kodi). Alishiriki katika ushauri sekta binafsi hasa kupunguza kodi, lakini hakuwahi kutegemea nyenzo hiyo ili kufaulu.

# Habari njema wanafunzi vyuo vikuu ujenzi hosteli

**Na Waandishi Wetu,**
DODOMA MJINI

SERIKALI imesema itajenga hosteli katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu (Duce) zitakazotumiwa na wanafunzi 2,280.

Vilevile, imesema itafanya upanuzi wa miundombinu ya makazi ya wanafunzi, utawezesha vyuo hivyo kupokea wanafunzi 6,120 kwa wakati mmoja na kuwaondolea wanafunzi kero ya mahali pa kuishi.

Habari hiyo njema ilitangazwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako jana bungeni jijini hapa, alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema UDSM litajengwa jengo la ghorofa mbili zaidi zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,280 katika Hosteli za Dk. John Magufuli na kwamba baada ya kukamilika kwa ujenzi huo, hosteli hizo zitakuwa na uwezo wa kupokea wanafunzi 5,120.

Alisema Duce watajenga hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 na kuiwekea samani

"Vilevile, wizara itaboresha hosteli za wanafunzi (NSSF Mtoni Kijichi) zenye uwezo wa kuchukua jumla wanafunzi 500," alisema.

Alibainisha kuwa kwa mwaka 2020/21, UDSM itadahili wanafunzi 29,056 wa shahada za awali pamoja na kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike kutoka 12,129 hadi 12,735 na kwamba ufadhili wa masomo utatolewa kwa wanafunzi 50 wa kike wanaosomea masomo ya sayansi.

Alisema serikali itaongeza idadi ya miradi ya utafiti kutoka 173 hadi 221 kwa kuwafadhili watafiti 40 katika maeneo yanayolenga uchumi wa viwanda na kuzingatia ajenda ya utafiti ya taifa.

Alisema Duce inatarajia kudahili wanafunzi wa mwaka wa kwanza 1,900 na kati yao, 600 ni wa fani ya sayansi.

Prof. Ndalichako pia alisema wizara yake imeandaa utaratibu wa wanafunzi kusoma kupitia redio na runinga kwa kipindi hiki walichopo nyumbani kutokana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (Covid-19).

"Tunawataka wazazi kuendelea kuwasimamia watoto wao kufuatilia masomo hayo kwa kipindi hiki wanachokuwa nyumbani,"alisema.

Akisoma maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Msemaji wa kambi hiyo katika wizara hiyo, Susan Lyimo, aliitaka serikali kubadili mfumo wa elimu kwenda kwenye mfumo wa kidijitali kupitia redio na runinga.

Alisema kambi hiyo inaona mfumo wa ufundishaji kwa njia ya redio na televisheni utasaidia wanafunzi kujifunza wakiwa majumbani na hivyo kujikinga na maambukizo ya corona kwa kuwa baadhi ya nchi zimetumia mfumo huo na umefanikiwa.

Lyimo pia alishauri bajeti ya elimu ipangwe kwa namna tofauti na miaka mingine ili kuzingatia hali halisi ya ugonjwa huo ambao umeathiri sekta ya elimu kwa asilimia 100.

"Itengwe bajeti ya kuendesha vipindi vya kitaaluma katika redio na televisheni, itengwe bajeti kwa ajili ya kutoa ruzuku kwa watoa huduma za intaneti ili kupunguza gharama za upakuaji wa mada, machapisho na vitabu mbalimbali vya elimu kwa wanafunzi,"alishauri.

Ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka ujao wa fedha, Profesa Ndalichako aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 1.3 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali wizara hiyo.

**Imaendikiwa na Salome Kitomari na Augusta Njoji, Dodoma**

## Polisi waendelea kuchunguza Amana

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limesema linaendelea na uchunguzi wa tukio la wagonjwa waliothibitika kuwa na virusi vya corona kudaiwa kutoroka katika Hospitali ya Rufani Amana jijini Dar es Salaam.

Kaimu Kamanda wa Kanda hiyo, Camilius Wambura, aliliambia Nipashe jana kuwa, bado wanaendelea kuchunguza tukio hilo baada ya juzi kupata taarifa za wagonjwa kutoroka hospitali hapo.

Juzi, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Sophia Mjema, alitoa ufafanuzi kuhusu taarifa za wagonjwa kudaiwa kutoroka Amana na kurejea nyumbani.

Mjema alisema kuna taarifa za wagonjwa hospitalini hapo za kulazimisha kuondoka ili kurejea nyumbani, lakini hakuthibitisha kuondoka kwao katika eneo hilo la matibabu.



Meneja wa Benki ya TPB PLC, tawi la Songea, Richard Chacha (kulia), akikabidhi cherehani 20 kwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Ruvuma, Jackline Ngonyani, kwa niaba ya vikundi mbalimbali vya wajasiriamali mkoani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC ahamishia shuleni familia zilizokumbwa na mafuriko

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KAYA 44 zimezingirwa na maji, huku familia 13 zikiwa katika hali mbaya wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro, kutokana na mafuriko makubwa yaliyoikumba.

Kutokana na baa hilo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya, amezihamishia kwa muda katika majengo ya Shule ya Msingi Sanya Station iliyoko Kata ya Kia kaya sita ambazo zina idadi kubwa ya watoto.

Jana, Ole Sabaya alisema: "Mpaka sasa tumefanikiwa kuzihamishia familia hizo shuleni, hali ni mbaya in kimsingi walio katika mahangaiko kutokana na mafuriko haya yanayotokana na mvua ya masika inayoendelea kunyesha kuzingira makazi yao, ni familia 44.

Kati yao, familia 13 ndiyo ambazo ziko kwenye hali mbaya na hawana kabisa makazi. Hili ni janga la asili, ndiyo maana nimesaidiana na maofisa wangu kuchukua hatua haraka kunusuru maisha ya wananchi," Ole Sabaya alisema.

Hali hiyo imesababisha baadhi ya familia kuyakimbia makazi yao na kutafuta hifadhi katika vitongoji vya jirani ili kuokoa maisha yao.

Kwa mujibu wa Ole Sabaya, familia zote zinazopambana na mafuriko hayo yanayotokana na janga la asili, zitahamishiwa maeneo salama ikiwamo kupata hifadhi kwa majirani zao.

Akizungumza na waathirika wa mafuriko hayo, Mkuu wa Wilaya huyo alisema kazi inayoendelea ni kufungua maji ya mafuriko na kuyaelekeza kwenda Mto Kikuletwa, kwa kuwa maji hayo yanayojaa eneo la Sanya Station kutokea milimani, yanatokana na wananchi kujenga eneo la asili ya maji.

Ofisa Kilimo wa Kata ya Kia, Maurin Mushi, akizungumzia mafuriko hayo, alisema zaidi ya ekari 175 za mazao mbalimbali, yakiwamo maharagwe, pilipili hoho na mahindi, zimeharibiwa vibaya kwa mazao hayo kusombwa na maji.

HABARI KITAIFA

# Madini Lindi yakusanya bil. 10/- miezi 15

**Na Saidi Hamdani,** LINDI

IDARA ya Madini mkoani Lindi, imekusanya maduhuri ya Sh. 10,338,512,791.29, baada ya wachimbaji wadogo kuzalisha kilo 99,618.38 za bidhaa hiyo kwa kipindi cha miezi 15 iliyopita.

Katika mgawo huo, Serikali Kuu imejipatia mapato stahiki ya Sh. 620,310,768.52 kutokana na mrabaha wa mauzo yake.

Kaimu Ofisa wa Madini mkoani humo, Jeremiah Hango, aliyaeleza hayo alipokuwa anatoa taarifa ya tathmini soko ya bidhaa hiyo, kwa Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, wilayani Ruangwa.

Hango alisema makusanyo hayo ni kuanzia Januari 2019 hadi Machi 20 mwaka huu, ambapo madini ya dhahabu na vito yalizalishwa na kuuzwa kwa kipindi hicho.

Hango alisema uzalishaji huo ni kutoka kwa wachimbaji wadogo kabla ya soko la mauzo kuanza, na kuwa baada ya soko, Serikali Kuu imelipwa mrabaha wa Sh. 620,310,768.52, wakati Sh.103,384,827.92 ni malipo ya tozo ya ukaguzi, huku Sh. 31,115,5,538.37 zikipelekwa kwenye tozo ya huduma.

Hango alisema kwa kipindi cha miezi mitano kabla ya soko kuanza Januari hadi Mei 2019, uzalishaji wa dhahabu na vito ni gramu 22.640.60, huku makusanyo yakiwa ni Sh. 1,871, 845,916.42. Alisema Serikali ikijipatia mrabaha wa Sh. 112,310,756.03, tozo ya ukaguzi Sh. 18,718,159.17 na Sh. 5,615,537.75 ikienda tozo ya huduma.

Alisema baada ya soko kuanzia Januari 2019 hadi Machi mwaka huu, uzalishaji ni gramu 76,977.78, na kuingiza maduhuri ya Sh. 8,466,666,874.87, huku Serikali ikijichukulia mrabaha wa Sh. 508,000, 012.49, tozo ya ukaguzi Sh. 84,666,668.75 wakati huduma ikiambulia Sh. 25,400,000.62.

Alisema pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Idara hiyo inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwamo watumishi, vifaa vya kupimia madini, mizani na uhaba wa wanunuzi kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19, ambapo nchi nyingi zimefunga mipaka yao.

Zambi aliwataka watumishi hao kuongeza jitihada kushawishi wanunuzi kutoka maeneo mbalimbali waende katika soko la madini lililopo Ruangwa kununua bidhaa hiyo.




Mhubiri maarufu kwa jina la Israel, akifanya maombi kwa ajili ya kuutokomeza ugonjwa corona katika eneo la Posta, mjini Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Waliozingirwa na maji Uvinza wapewa tahadhari

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

MKUU wa Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma, Mwananvua Mrindoko, amewaagiza wakazi wilayani humo kuchukua tahadhari ya usalama katika makazi ikiwamo maeneo yaliyo karibu na mito na Ziwa Tanganyika, baada ya nyuma zao kuzingirwa na maji.

Mrindoko alisema kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha wilayani humo, baadhi ya miundombinu imeharibika, kama barabara kukatika na maji kujaa katika mito, hivyo kusababisha wananchi waliojenga pembezoni ya mito na Ziwa Tanganyika nyumba zao kuzingirwa na maji.

"Niwaombe wote wanaoishi pembezoni mwa mito mikubwa na midogo waondoke mara moja waende kwenye maeneo ambayo yana usalama zaidi kwani kuna uwezekano wa maafa makubwa kutokea kwa watakaokaidi," alisema.

Hatua hiyo pia inatokana na mafuriko yaliyotokea katika Kata ya Ilagala wilayani humo ambapo nyumba nyingi zimezingirwa na maji na kulazimu wakazi wa maeneo hayo kutumia mitumbwi katika maeneo ambayo awali yalikuwa ni nchi kavu.

Johari Hussen, mmoja wa waathirika wa mafuriko katika eneo la Ilagala, aliiomba serikali kuwasaidia namna ya kuwahamisha katika eneo hilo kutokana na kuwa na hali duni ya kimaisha inayosababisha aendelee kukaa katika eneo hilo .

"Maji yametuvamia nilikuwa nasikia kuhusu mafuriko, lakini nimeyaona katika eneo letu hili ninatamani kuhama eneo hili, lakini shida kubwa ni pesa , tunaomba serikali itusaidie," lisema.

Maeneo mengi ya wilaya hiyo yameathirika na mafuriko kutokana na kuwa na mito mikubwa iliyojaa maji pamoja na kujaa kwa Ziwa Tanganyika na kusababisha baadhi ya wananchi kukosa makazi.

Naye Meneja wa Bonde Kanda ya Magharibi, David Manyama, aliwataka wananchi kuacha shughuli za kibinadamu karibu na vyanzo vya maji na kuitaja kama sababu inayochangia maji kuhama njia yake na kwenda kwenye makazi ya watu.

"Nitoe pole kwa waliokumbwa na mafuriko, lakini kila mwananchi anapaswa kufuata sheria za utunzaji wa mazingira kwani wengi wao wamekuwa wakaidi wa malekezo haya," alisema.

Pia Manyama alizitaka mamlaka zinazohusika kupima na kugawa viwanja kutokupima viwanja vilivyo ndani ya mita 60 kutoka kwenye chanzo cha maji kama mto au ziwa ili kuendelea kuhifadhi vyanzo vya maji katika uhalisia wake.

# Mmarekani anusurika kichapo madai ukaidi

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

RAIA wa Marekani ambaye hajafahamika jina lake, juzi alinusurika kipigo toka kwa wakazi wa Kijiji cha Safu wilayani Kalambo mkoani Rukwa, baada ya kulazimisha kuingia nchini kwa njia za panya kukwepa amri ya kukaa karantini kwa siku 14.

Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya siku moja kwa waandishi wa habari juu ya njia za kujikinga na maambukizi ya virus vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19.

Alisema mkoa huo unatekeleza njia mbalimbali za kujikinga na ugonjwa huo, ikiwamo ya mgeni anayeingia nchini kupitia mipaka iliyopo katika mkoa huo kutakiwa akae karantini kwa gharama zake kwa siku 14.

Wangapo alisema hivi karibuni kuna raia wa Marekani alikuwa anataka kuingia nchini kupitia mpaka wa Kasesya unaotenganisha Tanzania na Zambia, lakini alipofika mpakani akapewa taratibu ikiwamo kukaa karantini kwa siku 14 kwa gharama zake.

Baada ya kuelezwa sharti hilo, alikataa na kudai ni bora arudi Zambia kuliko kukaa karantini, na aliondoka na gari lake na kurudi Zambia alikokuwa anatokea.

Alisema alipofika mbele aliamua kubadiri njia na kuelekea katika Kijiji cha Safu kilichopo mpakani, akiwa na lengo la kuingia nchini kwa kutumia njia za panya, lakini alipofika katika kijiji hicho, wananchi walimzuia na kumtaka arudi Kasesya ili akafuate taratibu halali za kuingia nchini.

Wamgabo alisema mgeni huyo aliwagomea wananchi hao, kitendo kilichowaudhi na kukusanya mawe tayari kwa kumshambulia, lakini baadaye serikali ya kijiji hicho iliingilia kati na kumtaka Mmarekani huyo kurudi Zambia kwa usalama wake.

## KUMBUKUMBU



**Eng. Aloys Joseph Mwamanga.**

Familia ya Marehemu Mhandisi Aloys Joseph MWAMANGA wa Kunduchi Mtongani na Mbeya Block T. tunapenda kuwataarifu ndugu , marafiki na jamaa wote kuwa tarehe 25/04/2020 Marehemu atakuwa ametimiza mwaka mmoja toka alipotwaliwa , hivyo tutakuwa na misa ya Shukurani katika kanisa Katoriki Kunduchi Mtongani la Mt. Nikolaus Kuanzia saa Moja asubuhi. Kutokana na Hali ya ugonjwa wa sasa Covid-19 hatutakuwa na mkusanyiko baada ya Misa ya Shukurani. Tuna chukua nafasi hii kutoa Shukurani zetu za pekee sana kwa ndugu, Viongozi wa Dini, marafiki , wafanyakazi wenzake toka PEMACCO, TCCIA, TPSF, PPAA, NRCL, Mapembasi, Madakitari waliomuhudumia nchini Tanzania na India , Manesi walio mhudumia na jamaa wote walioshiriki na familia toka wakati wa kumuuguza na wakati wa mazishi yake huko Uwemba Njombe. Tunawaombea sana kwa Mwenyezi Mungu ili azidi kuwabariki na muwe na maisha marefu.

Kwa kweli nyinyi marafiki zetu wote , Wanajumuiya na majirani Dar es Salaam, Mbeya na Njombe, upendo wenu mlio tuonyesha hauna kifani , nasi hatuna cha kuwalipa. Mwenyezi Mungu awabariki sana

Unakumbukwa sana na mke wako, watoto wako na ndugu zako kwa busara, upendo, wema na upole wako!

**Raha ya Milele umpee e Bwana, na Mwanga wa Milele umuangazie, apumzike kwa amani.**

**Amina**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Simba isikimbizane na usajili Yanga, imulike Caf

**INGAWA** bado dirisha la usajili la Ligi Kuu Bara halijafunguliwa, klabu mbalimbali zinazoshiriki ligi hiyo hapa nchini, zimeanza kutumia fursa hii ya mapumziko yaliyotokana na mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19, kuanza kumulika huku na kule kuelekea dirisha hilo.

Lakini pia Ligi Kuu Bara bado haijamalizika na haijulikani ni lini itarejea kutokana na maambukizi ya virusi hivyo kuzidi kuongezeka na kufikia watu 299 kati yao 37 wakipona na vifo vikiwa 10 kutoka mgonjwa mmoja wakati serikali ikitangaza kusimama kwa shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo Machi 17, mwaka huu.

Hadi Ligi Kuu inasimama, Simba ndiyo iliyopo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 71, huku ikifuatiwa na Azam FC yenye alama 54 timu zote zikishuka dimbani mara 28, wakati Yanga ina pointi 51 zilizotokana na mechi 27 na Namungo ikifuata kwa pointi 50.

Hivyo, kwa ujumla Simba inahitaji pointi 11 katika michezo yake 10 iliyosalia kabla ya ligi hiyo kumalizika ili kuweza kutawazwa mabingwa kwa msimu wa tatu mfululizo. Kwa mantiki hiyo katika michezo 10 Simba iliyobakiza hata kama itacheza sare tisa na kushinda mechi moja tu, itakuwa imefikisha alama hizo 11 zitakazoiwezesha kufikisha pointi 82 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote ya Ligi Kuu Bara msimu huu.

Kimahesabu tunaamini endapo msimu huu hautafutwa kutokana na janga hilo la corona, na Ligi Kuu ikirejea hakuna timu inayoweza kuizuia Simba kutwaa ubingwa ambao hutoa tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika, michuano ambayo ina utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani humu.

Kwa klabu zilizosalia husussan zilizofuzu hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho nchini maarufu FA Cup, Yanga, Azam FC, Namungo FC, Ndanda FC, Kagera Sugar, Alliance FC na Sahare All Stars, zinapaswa kupigania kutwaa ubingwa huo ili kuweza kupata nafasi moja ya kuiwakilisha nchini kwenye michuano ya kimataifa kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika. Lakini pia, Simba na yenyewe ni miongoni mwa timu nane zilizofuzu hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.


Hiyo, inamaana uongozi wa Klabu ya Simba unapaswa kutulia zaidi katika mchakato wa usajili kwa kutazama idara zinazotakiwa kuboreshwa hasa kwa kutazama michuano ya kimataifa kwa kuwa kikosi cha chao cha sasa kama ni michuano ya ndani pekee, hata isipofanya usajili bado inaweza kutoa ushindani mkubwa katika Ligi Kuu.

Hivyo, hiki si kipindi cha kukimbizana na watani zao Yanga ama washindani zao, Azam FC katika mchakato wa usajili kwani klabu hizo mbili zenyewe hazijawa na uhakika hata kwa asilimia 50 kama mojawapo inaweza kutwaa Kombe la FA na kupata nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa kwa kuwa timu kama Kagera Sugar ama Namungo si za kubeza hata kidogo katika kinyang'anyiro hicho.

Tulishuhudia michuano ya msimu uliopita ambayo licha ya Simba kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali, ilipokea vipigo vya mbwa mwizi hususan ilipocheza ugenini dhidi ya Al Ahly ya Misri na AS Vita ya DR Congo kwa kupoteza kwa mabao 5-0 katika kila mchezo na kisha msimu huu ikitolewa mapema na UD Songo ya Msumbiji.

Hiyo inaonyesha wazi ni idara gani ambayo Simba inapaswa kuimulika zaidi katika usajili ujao ili kuweza kufuta aibu hiyo ya gharika ya mabao na kufika angalau nusu fainali ya michuano hiyo yenye ushindani mkali kwa ngazi ya klabu Afrika badala ya kukimbizana na Yanga na Azam katika usajili wa nyota wa ndani. Lengo letu ni kuiona ikimulika nyota wachache wa nje wenye uwezo na uzoefu wa michuano ya kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Dawa ya jipu kulipasua

Na Barnabas Maro

**MAANA** ya kichwa cha makala haya ni methali isemayo dawa ya jipu ni kulipasua na kulikamua. Twafunzwa umuhimu wa kukabiliana na hali fulani hata kama ni ngumu na kuimaliza. Mathalan mtu anapotakiwa kufanya uamuzi unaoelekea kuwa mgumu na ambao ni wa lazima una manufaa makubwa.

Mwandishi S.A. Ramadhani aliyeandika kitabu cha 'Vito vya Hekima, Simo na Maneno ya Mshangao', ameandika hivi:

"Donda ndugu liisha dawa." Kwamba mtu akielezwa na kunasihiwa juu ya jambo asitie vizibo vya masikio. Yaani mtu anayekakania (kakamaa) upotovu, hata akielezwa vipi hujitia hasikii, hakika yumo katika hasara ya kupuuzwa na wenziwe kama donda ndugu lipuuzwavyo.

Yote hiyo tisa, kumi ni hii: "Kukopa harusi kulipa matanga." Maana yake kukopa kuna furaha kama harusi, lakini kulipa ni msiba kama matanga. Methali hii huweza kutumiwa kwa mtu ambaye alikopa kwa bashasha, lakini akashindwa kulipa au ikawa anaona uzito au udhia kulipa!

Hivi ndivyo zilivyo klabu za mchezo wa kandanda nchini! Hata hivyo naizungumzia timu ya wananchi (Yanga) inavyokabwa koo na mchezaji wao wa zamani, Obrey Chirwa ambaye sasa ni mchezaji wa Azam FC.

Yanga ilimtwaa Chirwa mwaka 2016 kutoka FC Platinum ya Zimbabwe kwa makubaliano ya kulipwa dola 80,000 za Kimarekani. Baada ya mchezaji huyo kusaini mkataba na Yanga, akalipwa dola 70,000 akiahidiwa kumaliziwa dola 10,000 zilizosalia. Lini? Hiyo ni siri yao. Hata hivyo, fedha zingine anazoidai Yanga mpaka alipoachana nayo ni mishahara ya miezi mitatu yaani dola 12,000.

Chirwa alirejea tena nchini kwa lengo la kujiunga kwa mara ya pili na timu aliyoikimbia. Kama alikuwa na lengo hilo au kufuatilia kijanja fedha anazoidai Yanga, Allahu ya aalam (Mungu ndiye mwenye kujua zaidi).

Baada ya kuona anapigwa danadana kama mpira, akaamua kuishtaki klabu yake, Yanga, aliyoitumikia zamani. Alianzia TFF iliyompa barua kwenda ngazi za juu.

Chirwa anasema alipeleka malalamiko yake Shirikisho la Kandanda Afrika (CAF) lililomwelekeza kwenda FIFA. Huko walimpa barua ya kuwapelekea Yanga na kwa mujibu wa maelezo yake, aliwakabidhi viongozi husika.

Hapa ndipo penye 'kirumbizi' (kwa muktadha huu, ni ngoma inayochezwa na wachezaji inayohusisha kupigana kwa fimbo) kati ya Chirwa mdai, na mdaiwa yaani Yanga.

'Deni' ni kitu alichokopa mtu; jambo aliloahidi mtu kumfanyia mwingine; kitu au mali ambayo mtu anadaiwa. Ndo maana husemwa "Ahadi ni deni na deni ijuzie." Maana yake ahadi ni kama deni, mtu akitoa ahadi lazima aitimize. Methali hii yatufunza umuhimu wa kutimiza ahadi tutoazo.

Mvutano baina ya Chirwa na Yanga umesababisha Shirikisho la Kandanda Afrika (CAF) kuvitaka vyama vya nchi wanachama kutozipa leseni ya kusajili, klabu zinazodaiwa na wachezaji wao waliopo na wa zamani.

Kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almas Kasongo, utaratibu huu unaanza rasmi mwaka 2020/2021. Wakati huu klabu za kandanda zipo kwenye hekaheka za usajili wa wachezaji. Hapo ndipo penye 'songombingo' hasa. Itakuwaje kwa hao wanaotakiwa na klabu zenye madeni kwa wachezaji na wafanyakazi wao wa zamani?

"Tamaa mbele mauti nyuma." Ukiiweka tamaa mbele, mauti yatakuwa nyuma yakikufuata, utapatwa na mabaya. Methali hii huweza kutumiwa kwa mtu au watu wenye tamaa nyingi. Binadamu twafunzwa madhara yanayoweza kupatikana kutokana na tamaa isiyokuwa na mipaka.

Huu ni mtihani mgumu kwa viongozi wa klabu za kandanda nchini walio madarakani sasa. Je, walipoingia madarakani walielezwa na watangulizi wao kuhusu madeni yanayozikabili klabu zao? Walikaa pamoja kujua jinsi zilivyotumika fedha za klabu zao, orodha ya wachezaji na wafanyakazi wanaodai posho na mishahara yao pamoja na huduma za hoteli na usafiri timu zilipokwenda mikoani?

Kwa namna baadhi ya viongozi wa klabu za kandanda wanavyotumia hela za klabu mpaka wengine kuthubutu kusema eti 'kupiga pesa' (yaani kula hela) za klabu si vibaya, yanipa kichefuchefu! Hapa ni hela zitumiwazo kuwalipa wachawi ili eti kuzipa timu ushindi ilhali wachezaji ndiwo wanaoweza kuzipatia timu zao ushindi na si wachawi!

Kama wachawi hudhani kuwa wao ndiwo watoao ushindi, ni vema waanzishe timu zao waone kama watazishinda timu zinazofunzwa na walimu waliobobea huku wachezaji Wakristo wakimwamini mwokozi wao, Yesu Kristo na Waislamu wakimwamini Mtume Mohamed (SAW) waone kama watafurukuta (kitendo cha kiumbe hai kutotulia au kutikisika).



Watoto wakipita mtaani, huku wakiwa wamechukua tahadhari ya maambukizi ya vurusi vya ugonjwa wa corona kwa kuvaa vitambaa katika eneo la Segerea, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Corona yaitisha Tamwa kuelekea uchaguzi mkuu

**Na Mwandishi Wetu,**
ZAMZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa) Zanzibar, kimesema kinahuzunishwa na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Tamwa imesema virusi hivyo vinaendelea kuathiri maisha ya watu katika kipindi hiki cha mwaka wa Uchaguzi Mkuu wa 2020 nchini.

Mkurugenzi wa Tamwa Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, amesema kwa kushirikiana na wadau wengine kama Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar (JUWAUZA), Wanaume Wamabadiliko, kundi la Wazalishaji wa mawazo, TAMWA Zanzibar imeanzisha programu ya kuwaunga mkono wanawake kushika nafasi za uongozi katika Uchaguzi Mkuu ujao.

Mlipuko wa maradhi ya corona umeibuka wakati tukiwa katika hatua ya awali ya kuhamasisha jamii za Unguja na Pemba ili kuwakubali wanawake kama wagombea halali katika siasa za ushindani kama wenzao wa kiume.

Kwa hivyo, Tunatoa wito kwa jamii hasa wanawake, wanaume, viongozi wa dini na wanachama wa vyama vya kisiasa kuwaunga mkono wanawake kufikia matarajio yao ya kisiasa katika hali yoyote inayowezekana hasa wakati huu wananchi wanapohimizwa kuepuka mikusanyiko.

Alisema kwa mujibu wa mikutano ya uhamasishaji ambayo imefikia wadi 55 za Unguja na Pemba na kuzungumza na wanajamii 4,069, inaonekana kwamba wanawake wana uwezo mkubwa wa kuingia katika kinyan'ganyiko cha uongozi, ila wanakwazwa na tabia za baadhi ya wanajamii wanaoamini kuwa mwanamke hawezi kuongoza kwa mujibu wa dini ya kiislam. Mikutano hiyo ilifanywa na wanaume 22 wa mabadiliko kutoka Unguja na Pemba.

Baadhi ya viongozi wa dini wamekuwa wakitumia vibaya aya za Qur-an kuvunja moyo wanawake wanaotaka kugombea nafasi za uongozi, hali ambayo inapelekea wanawake kujitoa/kuacha kugombea nafasi za kisiasa

Viongozi hao pia huwa wanawataja mifano ya wanawake ambao wamepata nafasi kuwa viongozi wa umma na wanadhani wameenda kinyume cha maelekezo ya dini na hasa kwenye masuala ya ndoa.

Alisema viongozi hao wa dini hawakuweka suala hili katika muktadha sahihi, hivyo wamewakana wanawake kupata fursa sawa ya kukimbia pamoja na wenzao wa kiume.

Sheikh Abdalla Nassor Abdalla, kutoka Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA), Wilaya ya Chakechake, Pemba ambaye ni Mwanamme Mabadiliko, alisema jamii inahitaji kubadili mitizamo na mwazo dhidi ya mwanamke katika uongozi ili iweze kufaidi matunda ya wanawake.

Alisema uislamu haukupiga marufuku wanawake dhidi ya kupata nafasi za uongozi, hivyo aya maarufu inayotumiwa na viongozi wengi wa dini ambao mwanaume ni mlinzi wa mwanamke haimaanishi kuwa wanawake hawapaswi kushikilia au kugombea katika nafasi za uongozi.

Sheikh Abdalla alisema aya hiyo inasisitiza mwanamume kuwa mlinzi wa mwanamke.

"Kwa hivyo Tamwa Zanzibar tunawaomba wadau wote wa kisiasa kuwa makini katika kuzingatia mipango ya wanawake kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa 2020 kama mgombea halali katika kinyang'anyiro cha ushindi," alisema Dk. Mzuri na kuongeza:

"Hivi sasa wanawake saba tu ndio ambao wameshinda majimboni kupitia nafasi ya Uwakilishi sawa na asilimia 13 na wanawake wa tatu kati ya 50 ambayo wamepata nafasi ya ubunge kupitia majimboni Zanzibar sawa na asilimia sita.

Alisema sio sahihi kuwahukumu wanawake wagombea kwa makosa yaliyotendwa na wanawake wengine wakati wanaume hawahukumiwi kutokana na makosa ya wanaume wanzao.

"Kwa hivyo tunawaomba jamii kuheshimu wanawake kama watu waliyo na uwezo wa kuchukua uamuzi wao wa kujitegemea wakati ambapo wamepewa fursa ya kufanya hivyo.

Kwa mujibu wa Dk. Mzuri, wanawake wa Zanzibar wameonyesha uwezo mkubwa katika uongozi kutokana na ukaribu wao kwa jamii, kujitolea, wema, utulivu na uwajibikaji katika majukumu yao.

# Wizara yawezesha vijana ufugaji kuku

**Na Elizabeth Zaya**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imetoa vifaranga vya kuku 540 kwa kikundi cha vijana wajasiriamali, ili kuhamasisha ufugaji utakaosaidia kuziba pengo la uhaba wa nyama ifikapo mwaka 2022 pamoja na kukuza sekta ya kuku nchini.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Mazao ya Mifugo na Usalama wa Chakula na Lishe wa wizara hiyo, Gabriel Bura, alikabidhi vifaranga hivyo mwishoni mwa wiki kwa wawakilishi wa kikundi cha vijana watatu wajasiriamali jijini Dar es Salaam.

Bura alisema hatua hiyo inatokana na mkutano uliofanyika kati ya Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel na wadau wa tasnia ya kuku uliofanyika Machi 7, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Bura, Prof. Gabriel alishawishika na uwapo wa vijana wenye umri wa chini ya miaka 35 walioonyesha nia ya kuwekeza katika tasnia ya ufugaji wa kuku.

Alisema vijana hao wameonyesha uthubutu na wameonekana kupenda tasnia hiyo ili kukabiliana na hali halisi ya soko la ajira, akibainisha kuwa baadhi yao wamesomea fani za sheria na habari na mawasiliano.

Kwa mujibu Bura, mpango kabambe wa miaka 15 wa kuendeleza sekta ya mifugo umeonyesha kuwa kutakuwa na upungufu wa nyama kwa takriban tani 100,000 ifikapo mwaka 2022 kadri kipato cha wananchi kinavyoongezeka.

Alisema wameanza na Mkoa wa Mkoa wa Dar es Salaam na baadaye watakwenda wilayani Mkuranga, mikoa ya Mbeya, Morogoro na Dodoma na kwamba ni mchakato endelevu wa kutoa vifaranga kwa vikundi vya vijana wajasiriamali.

Sarah Urio. msambazaji wa viranga hivyo, aliwapongeza vijana kwa kuonyesha utayari na uthubutu wa kufuga kuku, akisema licha ya vijana hao kupewa vifaranga hivyo, uongozi wa kampuni yake utakuwa bega kwa bega kwa kuwapatia elimu ya namna ya kuendeleza shughuli hiyo ya ufugaji.


Enabel Belgian Development Agency

**CALL FOR EXPRESSION OF INTEREST**

**PROMOTION OF SANITATION AND HYGIENE IN KIGOMA**

The Kingdom of Belgium through Enabel and the Government of Tanzania through the Ministry of Water, are implementing a water and sanitation project in Kigoma region. This is a 5-year project which runs through June 2022 and aims to promote provision of sustainable water supply services in the region. The project now seeks to engage an NGO to carry out activities that aim at improving safe hygiene practices at household level in respective of: a) water collection, b) transport to point of use, c) storage d) use e) hand-washing and f) latrine use.

Interested NGOs can be local or international or a partnership of both but with a track record in carrying out sanitation and hygiene promotion activities using the most effective approaches. The project is looking for NGOs with capacity to implement and monitor and evaluate improvements in hygiene practices. Those organizations that are directly present or have implementing partners in Kigoma region will have an added advantage

More information and bid documents of this assignment are available at: **https://btctanzania.wordpress.com/**

21576201

TATEPA
**TATEPA PUBLIC LIMITED COMPANY**
*Company Registration Number: 24970*

**Notice of Postponement of the Annual General Meeting**

Notice is hereby given that the Annual General Meeting (AGM) of the Shareholders and Directors of Tatepa Public Limited Company the AGM which was to take place on 30th April 2020 has been deferred to 29th day of July 2020. The meeting will be held at same place and time on 29 July 2020 ie at The Courtyard Hotel, Ocean Road, Dar es Salaam at 09:30 hours.

This notice is hereby issued in line with the directives of Dar es salaam Stock Exchange complying to Government's directives that prohibits mass gatherings like meetings, in order to contain the spread of Coronavirus.

**Please be notified accordingly.**

**By Order of the Board**

**Vimalendu Kumar Tewari**
**Company Secretary**

**Dated at Dar es Salaam 23rd April 2020**

**Circulation:**

**To all members and Directors.**

215715601

# RC Ndikilo aonya wanaouza barakoa kwa bei kupindukia

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amewataka wafanyabiashara kuacha kujinufaisha kwa kuuza barakoa kwa bei ya juu ambayo wananchi wengine wanashindwa kumudu kununua.

Mhandisi Ndikilo alitoa onyo hilo alipokuwa akihamasisha wananchi wa Mailimoja, Loliondo, na stendi mpya kuvaa barakoa wakitoka nyumbani kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona. "Nitatembelea maduka ya dawa za binadamu kujua bei ya barakoa na nitaangalia wamenunua kiasi gani na wanauzaje, sitapenda kuona wafanyabiashara wakitumia ugonjwa huu kujinufaisha wakati wananchi wengine wanaumia na wanashindwa kumudu gharama za ununuzi," alisema.

Aliwataka wananchi kuhakikisha wanatumia barakoa sehemu yoyote kwa kuwa maambukizi ya ugonjwa huo yanaenda kasi na tayari katika mkoa huo wapo wagonjwa.

"Tuvae barakoa kila siku uwezekano wa kupata maambukizi ni mkubwa, tusidharau huu ugonjwa ni hatari tujikinge kwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya," alisema Ndikilo.

Alitoa wito kwa wananchi pia kutoa taarifa kwa kupiga simu wanapoona kuna mtu ana dalili zilizoainishwa na wataalamu wa afya kuhusiana na ugonjwa huo. Alisema, kuendelea kuwaficha wagonjwa ni moja ya chanzo cha kuzidi kuenea ugonjwa huo.

# CCM Ruvuma yakabidhi vifaa vya corona

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, amekipongeza chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani humo kwa kuona umuhimu wa kutoa msaada wa mashine tatu za kupima joto pamoja na vifaa vingine vikiwamo vitakasa mikono 20, vyenye thamani ya Sh. milioni tatu.

Mndeme alitoa pongezi hizo jana alipokuwa akikabidhiwa vifaa mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidia wananchi katika kupambana na ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona kutoka kwa Mwenyekiti wa CCM mkoa wa Ruvuma, Oddo Mwisho.

Alisema kuwa kitendo kilichofanywa na CCM mkoani hapa cha kuona umuhimu wa kutoa msaada wa ndoo 14, tenki tano za maji, sabuni 18 na vitakasa mikono 20 kinapaswa kuigwa na wadau wengine ili kuona namna ya kusaidia kupunguza kasi ya maambukizi ya ugonjwa huo.

Kwa upande wake Mwisho alisema jukumu la chama hicho ni kuhakikisha kuwa serikali inaungwa mkono kwa asilimia 100 kuutokomeza kabisa ugonjwa wa corona na aliwataka wananchi kuwa na tahadhari kwa kuepuka msongamano na safari zisizokuwa za lazima. Aliongeza kwamba vifaa vilivyolewa na CCM vipelekewe mahali ambapo kuna mikusanyiko kama sokoni, taasisi za elimu kama shule za msingi na sekondari pamoja na kwenye zahati, vituo vya afya na hospitali.

Katibu wa CCM mkoa wa Ruvuma, Nuru John Ngereja, alisema wanaendelea kutafuta uwezekano wa kupata vifaa vingine ili kusaidia kupunguza kasi ya maambukizi ya ugonjwa wa corona, na aliwahimiza wananchi kufanya kazi za maendeleo huku wakichukua tahadhari ya ugonjwa huo ambao umeshaingia mkoa wa Ruvuma.

TANESCO



Tuulinde Muungano wetu kwa faida yetu na vizazi vijavyo

tanesco_official_page umemeforum.blogspot.com tanescoyetultd tanescoyetu



# Wakulima mtama kunufaika na fursa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KITUO cha utafiti za mbegu bora za kilimo TARI Hombolo jijini Dodoma, kimeingia mkataba wenye thamani ya dola za kimarekani 11,000 na kampuni ya Bia Tanzania (TBL) kwa ajili ya kutafiti na kuzalisha mtama unaotakiwa katika kutengeneza bia.

Mkataba huo umefadhiliwa na Shirika la Afrika Kusini la AB INBEV.

Dk. Lammeck Makoe, ambaye ni mtafiti Mkuu wa TARI Hombolo Bwawani, alisema mkataba huo utasaidia kwa kiasi kikubwa sana katika kuzalisha mtama huo ambao unahitajia kwa ajili ya kuazalisha bia nchini.

Dk. Makoe alisema wao kama TARI wamefurahi kupata mkataba huo, huku akiwataka Watanzania kujiandaa kunufaika kwa fursa hiyo kutokana nchi kuwa na mbegu za mtama zilizo bora ambazo zitakuwa na soko kwa ajili ya kutengeneza bia.

"Tumefurahi kupata mkataba huo kwa sababu tunaamini utasaidia sana wakulima wa mtama kupata mbegu bora za mtama," alisema Dk. Makoe.

Alisema kilio cha wakulima ni kuhakikisha wanapata mbegu bora, hivyo mkataba huo ni neema kwao kwa sababu wana uhakika wa kuzalisha mbegu ambazo zinahitajika katika kuzalisha mtama huo unaohitajika kutengeneza bia.

Hata hivyo, alisema wakulima wanapaswa kuchangamkia fursa pale tu watakapoona mbegu hizo zimeanza kutolewa kwaajili ya watu kuanza kupanda mtama huo unaotakiwa kwa ajili ya bia.

Alifafanua zaidi kuwa, hivi sasa wakulima wa mtama watakuwa na uhakika kuwa wakilima mtama huo watakuwa na mahali pa kuuzia kutokana na TBL kuwa pamoja nao katika uzalishaji wa bia.

Naye Mkulima wa zao hilo, Juma Lubeleje, alisema wamekuwa wakihangaika na soko la mtama, lakini hivi sasa wanaamini soko lao litakuwa kwa sababu mahali pa kuuza kupo.

Alisema wanaishukuru TBL kwa kuonyesha njia baada ya kuingia mkataba huo na shirika hilo pamoja na TARI ambapo wanaamini watakuwa wakombozi wa wakulima katika eneo hilo.

"Tumefurahi sana kupata neema hii, tutajitahidi kulima kwa wingi ili

tuweze kuuza mtama ambao utatusaidia katika kuongeza kipato na familia zetu,"alisema Lebeleje.

Alisema yeye na wakulima wenzake wanasubiri tu mbegu hizo zitoke ili waanze kuzitumia katika kupanda na baadae wakati wa mavuno watakuwa na uhakika wa soko la mtama ambao unahitajika kutengeneza bia.

# Mbunge aipa BoT siri ya kununua dhahabu sasa, kuiuza baadae nje

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIKA kujihami na anguko la kiuchumi kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, Mbunge wa Msalala (CCM), Ezekiel Maige, ameishauri Benki Kuu Tanzania (BoT) kununua dhahabu kwa wingi, ili baadae wauze nje kwa faida.

Alisema kutokana na hali hiyo, kuna uwezekano wa uchumi wa dunia kutetereka, hivyo BoT kama watakuwa na dhahabu ya kutosha wataweza kuuza kwa bei nzuri itakayoipatia fedha za kutosha.

Alisema kutokana na ugonjwa huo, kuna mataifa makubwa uchumi wao umetetereka, hivyo kabla athari haijafika nchini, ni heri BoT wanunue dhahabu. "Dhahabu katika soko la dunia bado iko juu, ingawa katika soko la ndani imeshuka, hivyo BoT ingeangalia uwezekano wa kununua dhahabu nyingi ili baadae waweze kuuza na kupata faida kubwa," alisema Mbunge huyo.

Aidha, Maige alisema hivi sasa Ulaya dhahabu imepanda bei kwa kuwa wale walioweka hisa katika makampuni makubwa wanaanza kuuza kwa kuhofia anguko la kiuchumi, wanaona watapoteza fedha zao, hivyo wanaamua kununua dhahabu ili kuweka.

Aidha Mbunge huyo aliitaka Wizara ya Fedha kuingilia kati suala hilo, kwani lina maslahi kwa nchi, hivyo kujihami na anguko la kiuchumi kwa kununua dhahabu na kuhifadhi ni jambo jema. Maige alisema kuwa Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alipokuwa akiwasilisha bajeti ya Wizara yake, alisema suala la kununua dhahabu linafanywa na STAMICO, lakini hilo halizuii BoT nao kununua.

"Napenda kushauri ili suala la kununua dhahabu wasiachie sekta binafsi, BoT wanakaa na pesa nyingi, kwani badala kukaa na pesa, usikae na dhahabu ambayo ina thamani kubwa ambayo hata baadae ukiuza inakupatia fedha nyingi," alieleza Maige.

Maige alisema endapo serikali kupitia BoT watanunua dhahabu, wachimbaji wadogo watapata fedha, lakini pia itapata faida kubwa pindi watakapoamua kuiuza.




Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Athony Mavunde (kushoto), akikabidhi msaada wa vyakula vilivyotolewa na taasisi ya Dar-Ul-Muslimeen kwa kushirikiana na W.I.P.A.H.S, kwa ajili ya mfungo wa mwezi wa ramadhani kwa waumini wa msikiti wa Hudda Chamwino jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wanaonyonyesha watakiwa tahadhari dhidi ya corona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA


KINAMAMA wanaonyonyesha, wameshauriwa kuhakikisha wanajiweka katika hali ya usafi ili kujilinda na maambukizi ya corona yanayoweza kuwapata watoto.

Ushauri huo ulitolewa na Ofisa afya Mkufunzi kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Adolf Kinyunge, alipokuwa akitoa mafunzo kwa wanachama wa Chama cha Michezo cha Viziwi (DODSA) mkoani Dodoma.

Alisema kuwa ili kuwalinda watoto hao wanaonyonya, kinamama hao wanatakiwa kuhakikisha kabla ya kuwanyonyesha wanakuwa wasafi kwa ajili ya usalama. Ofisa huyo aliwatoa shaka kinamama hao kutokuwa na hofu ya kuwanyonyesha watoto hao kwa kuwa ni haki yao. Kwa upande wake, Toyi Midaba, ambaye pia ni Ofisa Afya Mwandamizi aliwataka wanachama hao wa chama cha michezo cha viziwi kuzingatia kanuni zitakazowafanya kuepukana na maambukizi ya ugonjwa huo hatari.

Alisema kutokana na mazingira waliyonayo, ni muhimu wakazingatia kanuni na maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya na viongozi wa serikali. Naye Mwenyekiti wa DODSA mkoa wa Dodoma, Japhaty Gama, alisema mafunzo hayo kwa upande wao yatawanufaisha na kutambua namna ya kuepukana na janga hilo.

Alisema pamoja na wao kukabiliana na changamoto nyingi kwenye janga hilo, pia watahakikisha wanatoa elimu kwa wezao ambao hawajatambua jinsi ya kuepukana na maambukizi ya ugonjwa huu.






Mkazi wa Iringa mjini, akisoma tangazo lililowekwa na ofisi za Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, linalozuia wananchi kuingia katika ofisi hizo bila kuvaa barakoa kama tahadhari ya maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa Corona. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Dk. Shein aonya wafanyabiashara bei

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

WAFANYABIASHARA nchini wametakiwa kuendesha biashara zao kwa uadilifu na huruma na wasitumie janga la Covid-19 kuwawekea mazingira magumu wananchi kuwapandishia bei kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, aliyasema hayo katika risala ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani aliyoitoa kupitia vyombo vya habari, ikiwa ni utaratibu wake aliouweka kila ukikaribia mwezi huo kila mwaka.

Dk. Shein aliwapongeza wafanyabiashara kwa kushirikiana na serikali katika kuhakikisha kwamba bidhaa zote muhimu hasa za chakula zinapatikana kama kawaida tangu yalipoingia maradhi hayo na kueleza matumaini yake kwamba hali hiyo itaendelea katika mwezi wa Ramadhani na miezi mengine inayokuja.

Aliwahimiza waumini wa dini ya Kiislamu kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kumtukuza pamoja na kusoma dua mbalimbali katika funga na sala zao za faradhi na suna katika mwezi wa Ramadhani na miezi mingine ili kuzidi kupata rehema na ulinzi wake. Aliwaeleza wananchi kuwa, mwaka huu wa 2020 mwezi Mtukufu wa Ramadhani unakaribishwa huku kukiwa na mtihani wa maradhi yanayosababishwa na virusi vya Corona.

Pia, alisisitiza kuwa, miongoni mwa mambo muhimu katika mapambano dhidi ya Covid-19 ni kujiepusha na mkusanyiko wa watu ingawa suala hilo limekuwa changamoto kubwa, lakini ni lazima litekelezwe kwa sababu mikusanyiko ndio njia mojawapo inayosababisha maambukizo. Alisema katika jitihada za kupambana na maambukizo ya maradhi hayo, kwa nyakati tofauti, viongozi mbalimbali wa serikali, madaktari na wataalamu wa afya, viongozi wa dini na taasisi mbalimbali wameendelea kuwaelimisha na kuwasihi wananchi kuhusu maradhi hayo.

Vile vile, alisema katika jitihada zilizochukuliwa na serikali, wananchi wameitikia wito wa viongozi mbalimbali na wamezingatia yote waliyoelimishwa na nasaha walizopewa katika kujikinga na maradhi hayo na kupunguza maambukizo yake.

Hata hivyo, alisema elimu zaidi inahitajika, ili iwafikie wananchi wengi zaidi waliopo katika maeneo ya Unguja na Pemba. Serikali na wahusika mbalimbali inapanga kuongeza kiwango cha taaluma, ili wanaonekana hawajazingatia vizuri elimu na taarifa zilizotolewa, waweze kuelimika zaidi. Dk. Shein alisema, serikali imelazimika kuongeza nguvu na uwezo wa kuyafuatilia, kuyashughulikia na kuyadhibiti maradhi hayo kwa kuendelea kutimiza wajibu wake na kuongoza mapambano dhidi ya maradhi hayo ambayo yanahitaji mchango wa kila mmoja.

# ZEC kupitia idadi majina, mipaka majimbo

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), katika kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka huu 2020 kwa mara nyingine inatarajia kufanya mapitio ya idadi, majina na mipaka ya majimbo ya uchaguzi yote mjini hapa.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mkuu mstaafu, Hamid Mahmoud Hamid, alisema kazi hiyo itafanyika kwa mujibu wa kifungu cha 120 (4) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambacho kimeipa uwezo Tume kufanya kazi hiyo kila ikifika kipindi cha miaka minane mpaka 10 au wakati mwingine wowote itakapoona inafaa. Alisema Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar mara ya mwisho ilifanya mapitio kama hayo ya majimbo mwaka 2015 kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015, ambayo yalisababisha kuongezwa kwa majimbo ya uchaguzi kutoka 50 yaliyokuwapo kabla na kuwa majimbo 54 yaliyotumiwa kwa uchaguzi wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

Alisema Tume hiyo imewajibika kufanyika tena mapitio ya majimbo hayo miaka mitano baada ya zoezi la mwaka 2015 kutokana na malalamiko katika baadhi ya majimbo ambako kuna wadi ambazo Shehia zake zinahudumiwa na majimbo mawili tofauti kinyume na utaratibu.

Alisema kwa kawaida kila jimbo linaundwa na wadi mbili mpaka tatu na kila wadi inaundwa na shehia mbalimbali zilizomo katika eneo la uchaguzi, katika kazi ya mapitio ya majimbo ya mwaka 2015, kuna mkanganyiko ulijitokeza katika wadi na majimbo ya uchaguzi Unguja na Pemba kutokana na hali hiyo, Tume imeamua kabla wa 2020 ifanye mapitio ya majimbo na ikiwezekana kwa mamlaka iliyo nayo ifanye marekebisho yanayostahiki kwa eneo ambalo linafanyiwa marekebisho.

Mwenyekiti huyo alisema, mapitio ya idadi na mipaka ya majimbo ya uchaguzi ni kazi shirikishi ingawaje mamlaka ya kufanya kazi hiyo kisheria ni ya Tume ya Uchaguzi.

Akizungumzia tathmini ya kazi ya uandikishaji na uhakiki wa taarifa za wapiga kura iliyomalizika hivi karibuni, alisema takwimu za awali zinaonyesha kuwa jumla ya wapiga kura 413,444 waliandikishwa na kuhakikiwa taarifa zao na kati yao wanaume walikuwa 199,327 na wanawake 214,117.

Alisema katika kuhakikisha kila mwananchi aliyekuwa na sifa anashiriki katika uchaguzi mkuu ujao, Tume imeandaa utaratibu maalum utakao wawezesha wananchi waliokosa fursa ya kuandikishwa katika daftari la kudumu la wapiga kura waweze kuipata. Tume hiyo ilisema ipo katika hatua za mwisho za upatikanaji wa vifaa vya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 pamoja na kuwafahamisha kuwa imekamilisha uchapishaji wa nyaraka, uagiziaji na ununuzi wa vifaa mbalimbali vya uchaguzi na baadhi vimeshakabidhiwa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi.

Hata hivyo, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilisema kwa kuthamini uwapo mkubwa wa wadau wa uchaguzi vikiwamo vyama vya siasa, asasi za kiraia na mtu mmoja mmoja, inatoa nafasi kwa wadau wote kushiriki kikamilifu kutoa maoni na maono yao kwa njia ya barua au mawasiliano yoyote kwa Tume ya hali ya majimbo kuelekea uchaguzi mkuu.

Tume haitoandaa mikutano ya maoni, badala yake itapokea maoni na maono hayo kwa njia ya barua katika Ofisi Kuu ya Tume ya Uchaguzi iliyopo Maisara Unguja, Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Pemba iliyopo Chake Chake au katika Ofisi za Wilaya za Tume zilizopo katika wilaya zote za Unguja na Pemba ili kuepuka mikusanyiko.

# Maliasili yakamata roli 6 zikichimba mchanga

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka Zanzibar, Sudi Mohmed Juma, amesema Idara hiyo itaendelea na operesheni ya udhibiti na uhifadhi wa mazingira hasa katika Wilaya ya Kaskazini A Unguja kutokana na kukithiri kwa uharibifu wa mazingira.

Aliyasema hayo wakati alipokuwa akitoa taarifa za gari sita za mchanga na gari nane za ng'ombe zilizokamatwa zikiwa zinachimba mchanga katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Alisema kutokana na operesheni hizo, Idara imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kudhibiti maeneo ambayo sio rasmi kuendesha shughuli hizo za uchimbaji mchanga ambayo yalikuwa yakitumika kama machimbo ya kawaida mitaani na kusababisha uharibifu wa mazingira.

Alisema licha ya Idara hiyo kuendelea kuchukua hatua katika kudhibiti vitendo vya uchimbaji mchanga kiholela, katika maeneo ya wazi na makazi, bado baadhi ya jamii haitaki kuwafichua wanaondesha vitendo hivyo katika maeneo yao jambo ambalo linarudisha nyuma juhudi za kuhifadhi mazingira hususani katika maeneo ya makazi ya watu.

"Kama kipindi hiki cha mvua limezuka wimbi la baadhi ya wananchi kuchimba mchanga kiholela katika maeneo mbalimbali ya makazi yao, muda mwingine unasababisha hata kutuwama maji katika makazi yao, hili ni jambo hatari, wao hawaoni athari kwa kipindi kile lakini athari yake kubwa baadaye kwa kuwa usababisha mashimo ambayo yana uwezo wa kujichimba chini kwa chini kila mvua itakaponyesha," alisema.

Hivyo aliwataka wananchi kushirikiana na viongozi wa idara hiyo kwa kutoa taarifa pindi wanapoona uharibifu wowote wa maliasili ili kutimiza lengo la idara hiyo la uhifadhi na udhibiti wa maliasili na mazingira.

Akizungumzia uharibifu wa ukataji miti kwa kutumia misumeno ya moto, Mkurugenzi huyo alisema zaidi ya misumeno 40 wamekamata na wanatarajia kuiteketeza ili kuondoa uharibifu wa mazingira kwani bado baadhi ya wananchi wamekuwa wakiharibu mazingira kwa kukata miti kwa kutumia msumeno hiyo na kinyume cha utaratibu uliyowekwa.

Msimamizi wa sheria kutoka Idara ya misitu, Haji Haji alisema gari hizo zimekamatwa katika maeneo mbalimbali na watahakikisha wanawachukulia hatua za kisheria watu waliokamatwa na maliasili hizo.



**YEMI ALADE UNAICHOKONOA SERIKALI, SHAURI YAKO** Ukurasa14



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT



INASIKITISHA

# Gigy Money anaelekea kudata

INASIKITISHA! Ndivyo mashabiki wa mwanamuziki na mpambaji wa video za muziki, Gigy Money, wanavyosema baada ya hali ya msanii huyo kubadilika siku hadi siku.

Wiki hii Gigy Money aliachana na mpenzi wake Hunchy Huncho, na kuibua kizazaa kutokana na kuonekana kama ameathirika kisaikolojia.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram live, Gigy alionekana akimlalamikia mpenzi wake huyo kwa kutomuheshimu mama yake licha ya yeye kumuhudumia kila kitu.

"Hata kama nampenda lakini hawezi kumtukana mama yangu, yeye namhudumia kila kitu hilo hajali kabisa, basi wacha aende,"alisikika Gigy akilalamika huku akilia.

Hata hivyo, haikupita siku tatu alifuta picha zote katika akaunti yake na kisha kubakisha posti ambayo iliwapa mashaka mashabiki wake baada ya kusema hawezi kuamini kinachomtokea, anaona anajichukia mwenyewe na amekuwa dhaifu.

"Natamani kufariki bila sababu yoyote, siwezi kula wala siwezi kulala kwa kifupi siamini na hii imezidi, sasa najichukia mimi mwenyewe na nimekuwa dhaifu, yaani inauma ila inabidi uwe mkubwa kuelewa, sipo "interested" na mtu yeyote yule wote wamenishinda nimechoka" ameandika Gigy Money.

Baada ya kuweka post hiyo, mashabiki wake walimtahadharisha wakimwambia ajikaze kwani anaweza kuathirika kiakili.

Gugy ameonekana akimwaga chozi huku akijilaumu na kutoamini kile kilichomtokea mpaka kuachana na mpenzi wake.

BASI SAWA

## Duh! Barakah unaweza kutembeza rungu

MWANAMUZIKI, Barakah The Prince, amezidiwa na wivu kiasi ambacho sasa anamiliki akaunti ya Instagram ya mpenzi wake kuchunguza nani anamnyatia.

Ukurasa wa mpenzi wake huyo wenye jina la Najdattan, huchunguzwa kila wakati na pale akiona ujumbe wa kimahaba kutoka kwa mwanaume, basi yeye huchukua hatua ya kuruka naye hewani.

"Huyu ni mke wangu ila bado ndoa tu ili kukamilisha kwa sababu familia yake inajua kwamba naishi naye kwangu, huwa nashika simu yake na namiliki akaunti yake ya mtandao wa Instagram ila sijawahi kuona ametumiwa ujumbe kutoka kwa msanii, ila siku masela wakijichanganya utaona naruka naye mmoja" ameeleza Barakah The Prince.



## Dully Sykes mke hupangwa na Mola

MUIMBAJI mkongwe wa BongoFleva, Dully Sykes, amefunguka akisema bado hajamuona mwanamke aliyepewa na Mungu kwa ajili ya kufunga naye ndoa.

Akizungumza na EATV, Dully amesema kila kitu anachokifanya anamtegemea Mungu na hata suala la mke atafanya kama ndugu yake, Q Chief, ambaye amepata mwenza hivi karibuni.

"Inshaalah nitafunga ndoa na mke bora analetwa na Mungu, kwa sababu ndoa huipangi wewe inapangwa na Mungu, ukitaka kujipangia mwenyewe utaoa leo kesho utaacha, kwahiyo mimi nitakuwa kama ndugu yangu Q Chief nasubiri Mungu aniletee jiko nitaoa"amesema Dully Sykes.






# Harmonize umeingilia mahaba ya TID?

MAMBO hadharani! Pamoja na Staa wa muziki wa Bongo Fleva, Harmonize, kuweka hadharani mapenzi ya wasanii wenzake TID na Lulu Diva, sasa ameanza kugeukwa akidaiwa kufanya umbea kwenye mahaba ya watu.

Harmonize ndiye aliyewaaminisha watu wengi baada ya kuposti video fupi ikiwaonesha wamejirekodi wimbo wake kisha akaandika "Mahusiano ninayoyapenda kwa sasa, washaanza kufanana mapenzi ni matamu"

Hapo ndipo TID alipoamua kuzungumza na EATV, akisema Harmonize ni mtoto mdogo hapaswi kujua yeye anachokifanya.

"Konde Boy ni kijana hakuna mfano naye, anaweza akasema chochote na siwezi ku-comment chochote lakini hapaswi kujua, japo alichokisema kinaleta maana ila siwezi kubishana na mawazo yake ila akumbuke kwangu yeye bado ni mtoto mdogo". amesema

# Haki yangu; Haki ya mtu haipotei

**Na Adam Fungamwango**

HAKI yangu, ni filamu ya kusikitisha, ambayo inatufundisha kuwa kosa la mtu mmoja linaweza kusababisha matatizo kwa watu wengine wasiohusika, lakini wenye nasaba na mtu aliyefanya kosa.

Lakini pia inatuonyesha kuwa haki ya mtu haipotei, itakata kona, itazunguka, lakini mwisho wa siku itarudi kwenye sehemu ya halisi ilipotakiwa iwe.

Imechezwa na wasanii wengi, wakiwamo maarufu kama Emmanuel Mapunda, Mohamed Mwikongi, Hasim Kambi, Charles Njama, Soud Ally, Khadija Abdallah, Jackson Joseph na wengineo.

Baada ya kumaliza shule ya msingi, Meriana anashindwa kuendelea na masomo ya sekondari kwa kukosa ada. Anaishi na mama yake pekee, lakini mara kwa mara akimuulizia baba yake anaambulia kichapo. Kitendo cha kutoendelea na masomo kinamkera na kumlazimisha mama yake Devota amtajie baba yake, ili amtafute kwa ajili kumlipia ada. Mama yake anaamua kujiua. Anaandika barua kuwa amemua kufanya hivyo kwa sababu aliweka nadhiri kuwa binti yake huyo hawezi kumuona baba yake akiwa hai. Na hii inatokana na jinsi alivyomfanya siku za nyuma. Devota akiwa hausigeli, alibakwa na baba mwenye nyumba mzee Mangushi.

Baada ya kupata ujauzito akafukuza kama mbwa, akamzaa na kumlea binti huyo kwa tabu, ndiyo maana aliiweka nadhiri hiyo. Hata hivyo akampa ramani ya kwenda kumtafuta baba yake.

Meriana anaingia jijini Dar es Salaam, kumtafuta baba yake, na kwa bahati nzuri anaangukia mikononi mwa Mapunda, Mwanasheria wa baba yake mzee Mangushi. Mwanasheria huyo baada ya kupata maelezo yaliyojitosheleza na yenye ushahidi usiotia shaka, alithibitisha kuwa binti huyo ni wa mzee Mangushi.







# Ali Kiba umenena kibusara

MAFANIKIO huja kwa kutumia njia mbalimbali, lakini kwa Ali Kiba, anaamini mambo mawili yanaweza kuinuliwa kisanii.

Akizungumza na EATV, amesema watu wanaweza kufanikiwa kutokana na bahati, lakini inachagizwa na uwezo wa mtu husika.

"Kuna muda unatakiwa kuwa na bahati, ila lazima uwe na uwezo pia kwa sababu bahati huwa inamchagua mtu, vilevile kuna watu wana uwezo lakini hawana bahati, kwahiyo tunahitaji bahati kwenye maisha yetu maana ukiwa na nguvu ya bahati hakuna hata mtu mmoja ambaye ataweza kukupa changamoto" amesema Alikiba.

# Zuchu alianza kama hawa

**Na Adam Fungamwango**

HABARI ya mjini kwa sasa ni msanii mpya wa kike kwenye muziki wa kizazi kipya Zuhura Omari ambaye kwa jina la kimuziki anajulikana kama Zuchu.

Waswahili wanasema mvumilivu hula mbivu, baada ya kusota, tayari ameanza kuteka hisia za mashabiki wa muziki huo nchini na nje ya nchi kwa sasa.

Zuchu ambaye ni binti wa mwimbaji wa nyimbo za taarabu, Malkia wa mipasho, Khadija Kopa kwa muda mfupi tu ameingia kwenye anga za muziki kwa nyota kali, na kutabiriwa makubwa kwenye tasnia hiyo.

Kwa siku za karibuni, ameanza kwa kutoa ngoma kadhaa ambazo karibuni zote zimedondokea kupendwa na mashabiki.

Ngoma hizo ni 'Mauzauza' aliouimba na mama yake, ukiwa kwenye mahadhi ya mduara, 'Ashua' alioimba na Mbosso, 'Wana', 'Kwaru', na 'Hakuna Kulala.'

Hii imekuwa ni kawaida, kila baada ya muda fulani anatokea msanii wa kike na kuanza kutamba na kutishia wenzake kwenye fani hiyo ya muziki.

Hawa ni baadhi ya wasanii ambao nao waliwahi kuibuka na kufunika anga la muziki wa kizazi kipya.

**LADY JAYDEE**

Ni mmoja wa wasanii mwanzo wa kike kwenye kizazi cha bongo fleva.

Mwaka 2000, Lady Jaydee alitoa albamu yake ya kwanza aliyoiita machozi iliyokuwa na nyimbo tisa zilizomfanya kuwa msanii wa kike aliyetikisa kipindi hicho.

Mwaka 2003, msanii huyo ambaye jina kamili ni Judith Wambura, alifunga kazi alipoachia albamu ya pili iitwayo 'Binti', iliyokuwa imesheheni ngoma zilizoondokea kupendwa mno kama 'Usiusemee Moyo', 'Siri Yangu', 'Wanaume kama Mabinti' na nyinginezo.

**KEISHA**

Miaka michache tu baadaye, wakati Lady Jaydee akitamba, aliibuka msanii mpya wa kike, Khadija Shaaban, aliyejulikana kwa jina la 'Keisha'.

Huyu naye aliibuka kwa kishindo kama cha tembo porini.

Aliibuka na ngoma zake zilizotetemesha anga la muziki wa Tanzania, kama 'Uvumilivu', 'Huruma' alioimba na Bushoke, pamoja na 'Zawadi ya Pendo.'

**RACHEL**

Kwenye miaka ya 2010 hivi, aliibuka mrembo mmoja mkali aitwaye Rachel. Kwa bahati mbaya akawa mmoja wa wasanii wa kike waliodumu au kuvuma kwa muda mfupi sana.

Alitingisha mno na ngoma yake kali aliyoiita 'Kizungu-zungu' na baadaye 'Nashukuru Umerudi.'



**RAY C**

Kuna msanii mmoja aitwaye Reheme Chalamila, naye kwa wakati wake aliibuka kwenye miaka hiyo na kutetemesha anga la muziki wa bongo fleva, si tu kwenye uimbaji wake, lakini pia uchezaji na kutungwa jina 'kiuno bila mfupa.'

Alotamba na ngoma zake kama, 'Wanitafutia Nini', 'Na Wewe Milele', 'Unanimaliza', 'Sikuhitaji' na nyingine nyingi.

**NANDY**

Mwaka 2013, aliibuka msanii mwingine wa kike ambaye ndiye kwa sasa anaendelea kuwa tishio, kabla ya ujio wa Zuchu. Anaitwa Nandy. Kwa sasa anapigania ili umalkia wake usipotee kwa msanii mpya Zuchu.

Ngoma zake kali zilizofanya kuwa malkia ni 'Kivuruge', 'Ninogeshe', 'Na Nusu', 'Kata', 'Kiza Kinene', 'Nikukumbushe' na nyinginezo.



# Kelly kama kweli kubali yaishe

MCHEZA filamu wa Nigeria, Kelly Hanspme, amepinga madai ya mama wa mtoto wake, Ronke Moredeyo, kwamba alimtumia ujumbe wenye vitisho.

Kelly na mwanamke huyo ambaye ni mama wa mtoto wake, wamekuwa katika mgogoro mzito huku akimtuhumu kumpa vitisho.

"Hakuna mwanamke mwenye akili zake sahihi atakayekushambulia. Sijakaribia kupaka uchafu kwenye matope lakini unaona hii ngoma ya fedheha uliyoianza, uwe tayari kusimulia hadithi wakati ulipotakiwa kujibu," ameandika Kelly katika ukurasa wake wa Instagram.



## Yemi Alade unaichokonoa serikali, shauri yako

MWANAMUZIKI Yemi Alade, ameamua kuwafungukia viongozi wa serikali akiwataka kueleza misaada iliyotolewa kupambana na ugonjwa wa COVID 19 kama imeleta matokeo chanya katika jamii.

Yemi Alade ametoa wito huo kwa mamlaka ya jiji la Lagos na shirikisho kueleza namna pesa hizo zilizochangwa na wafadhili zilivyotumika katika kupambana na ugonjwa huo.

"Mheshimiwa Buhari, kuna maswali yanayotawala kuhusu zaidi ya Bilioni 25 kupambana na COVID 19, mbona hakuna uwazi wa matumizi yake?" aliuliza.

## Chioma upo sawa mrembo

MCHUMBA wa mwanamuziki nyota wa Nigeria, Davido, amemaliza muda wake wa karantini kwa kuanza kuwapa ushauri wanawake wasiwe tegemezi kwa wanaume.

Chioma Rowland, ambaye tayari ana mtoto mmoja na Davido, amemwambia shabiki yake mmoja wa kike kwamba asipoteze muda kumsubiri mwanamume, kwani yeye mwenyewe anaweza kusaka maisha.

Mrembo huyo ambaye alikutwa na virusi vya COVID 19 aliungana na familia yake siku chache zilizopita baada ya kufanyiwa vipimo na kugundulika hana ugonjwa huo.





## Duh! Kwa hili Kylie umepinda

MWANAMITINDO na bilionea, Kylie Jenner, wiki hii amejikuta akivunja amri ya kutotoka nje baada ya kwenda Beverly Hills, kumtembelea rafiki yake Stassie Karanikolaou.

Marekani imeweka kizuizi kwa raia wao kubaki nyumbani kujilinda na virusi vya corona, lakini Kylie aliamua kutoka nyumbani kwake akiwa hana vipodozi kwenye sura yake ili kuwaadaa polisi.

Mashabiki wake walishangazwa na tukio hilo, lakini yeye aliwapa ushauri kutomuiga na badala yake wapaki ndani ya nyumba zao.

## Uriel Oputa umetisha sana

ALIYEKUWA mshiriki wa shindano la Big Brother Nigeria (BBNaija), Uriel Oputa, amemjia juu mwanamume mmoja ambaye amepiga mtoto wake baada ya kufeli masomo.

Uriel, amesema video inayosambaa mitandaoni ambayo inamuonyesha mzazi huyo akimchapa mtoto wake, haipaswi kuungwa mkono kwa sababu haifundishi malezi mema.

Mzazi huyo kutoka nchini Zambia alirekodiwa akimchapa mtoto wake kama adhabu baada ya kufeli masomo yake shuleni.



MAKALA

# MAJARIBIO DAWA CORONA YAFELI

## ■Wagonjwa waliopewa China haikuwasaidia

IKIWA Dunia imetaharuki, kila nchi ikijitahidi kukabiliana na mlipuko wa COVID 19, kwa mara ya kwanza matumaini ya kupata dawa ya kupambana na virusi vya corona yameanza kupotea, baada ya majaribio yake kushindwa kufanya kazi.

Dawa hiyo ambayo ilitazamiwa kutibu virusi vya corona inaripotiwa kushindwa kufikia viwango vya ufanisi katika jaribio lake la kwanza.

Kwa mujibu wa Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), awali kulikuwa na matumaini dawa hiyo inayoitwa remdesivir ingeweza kutibu ugonjwa wa virusi vya Covid-19.

Hata hivyo, katika jaribio la dawa hiyo lililofanyika nchini China, limeonyesha hakuna mafanikio kama ilivyogundulika kupitia waraka wa siri uliochapishwa kimakosa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Katika waraka huo unaeleza kwamba, dawa hiyo haikuboresha afya za wagonjwa au kupunguza kiwango cha virusi kwenye damu zao.

Pamoja na matokeo hayo ya kuvunja moyo, kampuni ya Marekani inayotengeneza dawa hiyo, Gilead Sciences, imesema kuwa waraka huo ulipotosha uchunguzi wake.

Taarifa juu ya kushindwa kwa jaribio la dawa hiyo ilisambaa mitandaoni na baadae kuondoa data hizo.

Shirika hilo limekiri kwamba ripoti hiyo ya muswada iliwekwa mtandaoni kimakosa.

Taarifa hiyo inaonyesha kuwa watafiti waliwafanyia uchunguzi wagonjwa 137, wakawapatia dawa 158 na kulinganisha mafanikio na waliosalia 79, ambao walipewa dawa isiyo na kemikali ya placebo.

Baada ya mwezi mmoja, asilimia 13.9 ya wagonjwa waliokuwa wakipokea dawa hiyo walikufa ikilinganishwa na asilimia 12.8 ya wale waliopokea placebo.

Kutokana na matokeo hayo, jaribio hilo lilisitishwa mapema kwa sababu ya madhara yake yalionekana makubwa.

"Remdesivir haikuhusishwa na faida za kimatibabu wala za uchunguzi wa virusi ,"ulieleza muhtasari wa waraka huo.

Baada ya kuonekana kwa ripoti hiyo, viwango vya hisa vilishuka haraka katika masoko makuu matatu ya hisa nchini Marekani kwa zaidi ya asilimia moja ya faida .


Hata hivyo, kampuni ya Gilead imepingana na taarifa ya WHO, ikisema data zilizowekwa hazikuwa sahihi na kwamba walisitisha utafiti kutokana na watu wachache kujitokeza.

"Tunaamini kuwa taarifa iliyotumwa ilikosewa data kuhusu utafiti," msemaji wa kampuni ya Gilead anasema.

Anasema utafiti huo ulisitishwa mapema kutokana na kujitokeza kwa watu wachache walioshiriki na hivyo takwimu zake hazikuwa na maana.



Madaktari wakimuhudumia mmoja wa watu waliopata maambukizi ya corona




Moja ya sampuli ya dawa iliyofanyiwa uchunguzi wa kutibu COVID 19

"Kutokana na tatizo hilo, matokeo hayakukamilika ingawa kile kilichojitokeza katika data kinaonyesha uwezekano wa faida ya dawa ya remdesivir, hususani miongoni mwa wagonjwa waliotibiwa katika hatua za mapema za ugonjwa," anaisema.

Pamoja na kuibuka kwa utata huo, kampuni hiyo inaeleza kwamba huo sio mwisho wa safari wa kutafiti dawa hiyo , kwani majaribio kadhaa yanayoendelea yatatoa picha halisi ya matumizi sahihi ya dawa hiyo.

Zaidi ya dawa 150 zinafanyiwa utafiti duniani.

Nyingi kati ya yazo ni dawa zilizopo ambazo zimekuwa zikifanyiwa majaribio dhidi ya virusi hivyo.

Shirika la Afya Duniani WHO limezindua majaribio ya pamoja ili kuchunguza tiba yenye matumaini.

Uingereza inasema kwamba majaribio yake ndio makubwa zaidi duniani huku zaidi ya wagonjwa 5000 wakishiriki.

Na vituo vingi vya utafiti duniani vinajaribu kutumia damu ya waliopona kama dawa.

UTAFITI MWINGINE

Kuna aina tatu za dawa zinazofanyiwa uchunguzi kuona kama zinaweza kukabiliana na virusi vya corona.

Pia Chloroquine na Hudroxychloroquine zinaweza kuwa na uwezo wa kukabiliana na virusi hivyo na kuzuia kinga za mwili kushambuliwa.

Dawa hizo zimepata umaarufu kama mojawapo ya tiba za corona, kutokana na madai yaliotolewa na Rais Donald Trump.

Hydroxychloroquine pia hutumika kama tiba ya ugonjwa wa baridi yabisi kwa kuwa inaweza kusaidia kinga mwilini.

Majaribio katika maabara yameonyesha kwamba inaweza kuzuia virusi hivyo na kuna ushaihidi kutoka kwa madaktari unaosema inaweza kuwasaidia wagonjwa.

MAKALA

# Nyota Njema: Vijana wanaotimiza ndoto kusaidia kaya masikini

**Na Moshi Lusonzo**

VIJANA ni moja ya kundi kubwa katika jamii ambao wana uwezo mkubwa wa ushawishi katika kupanga na kutekeleza mipango mbalimabli na kuleta matokeo chanya.

Hii inatokana na nguvu walizonazo katika kutumia elimu, vipaji na utendaji wao kazi. Wapo walioongoza kwenye mabadiliko ya kisera, kiuchumi na kisiasa na kufanikiwa kuiweka jamii pamoja na katika mshikamano wa hali ya juu.

Jumuiya ya vijana na Nyota Njema, ni sehemu ya vijana ambao wameamua kutumia uwezo wao wa kifikra, kiuchumi na kielimu, kuhakikisha watu wanabadilisha mtazamo na kuona wana wajibu wa kuwapa matumaini watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Kupitia miradi yao tofauti, vijana hao wamewanufaisha watoto kutoka kaya zaidi ya 80, kuwa na uhakika wa chakula, elimu kwa watoto na huduma ya bima ya afya.

Miradi mingine wanayoitekeleza ni utunzaji wa mazingira, usaidizi kwa wagonjwa hospitali, kuwarudisha shuleni watoto wanaoishi mazingira magumu.

Akizungumza na gazeti hili, Mweka Hazina wa jumuiya hiyo, Hemed Lumeme, anasema Nyota Njema ilianzishwa kutokana na mawazo ya vijana hao, ambao walikuwa na ndoto ya kuona jamii inaishi katika usawa kwa wale wenye fedha na wasio nacho.

Anasema katika kutimiza ndoto yao, wanatumia rasilimali zao na kuomba ufadhili katika taasisi zingine ili kupata fedha kwa ajili ya kugharamikia miradi hiyo.

Katika muda wa miaka minne, wameanza kupata mafanikio baada ya kuwafikia watu wengi ambao kimsingi wanahitaji kuongezewa nguvu kuendesha maisha yao.

"Tulikuwa na ndoto ya kuona jamii inaishi pamoja kwa furaha bila kuwapo na mipaka ya matajiri na maskini, sasa tumenza kuona mafanikio baada ya kuwarudishia matumaini na furaha kwa idadi ndogo ya jamii tulizozifikia," anasema Lumeme.

Anasema katika mradi wa ugawaji wa chakula kwa kaya zinazoishi katika mazingira magumu, mwaka huu pekee zimetumika zaidi ya milioni sita ambazo zimewanufaisha familia 49 ndani ya jiji la Dar es Salaam.

"Tunatembea kila nyumba ambayo ina walengwa kuwapa kile tulicho nacho, nafurahi kuona kwa mwaka huu tumekwenda mbali zaidi baada ya mwaka uliopita tuliwafikia kaya 30 pekee," anaongeza kusema.

Ofisa Rasilimali Watu wa Jumuiya hiyo, Said Zahran, anaeleza kwamba pamoja na mradi huo wa ugawaji chakula, pia wamefanikiwa kuwarudisha shule watoto 50 ambao walishindwa kuendelea na masomo kwa kukosa pesa.

Anasema katika mradi huo unaojulikana kama 'Rudi Shuleni' wanajitolea kuwahudumia watoto walioshindwa kuhudhuria shuleni kutokana na wazazi wao kutokuwa na uwezo.

Zahran anaeleza kuwa katika mpango huo, watoto ambao wamekatisha masomo kutokana na sababu za kiuchumi wanapatiwa msaada wa madaftari, vitabu vya kiada na ziada pamoja na sare za shule.

"Tumegundua watoto hawa wana nia ya kusoma, lakini kutokana na wazazi wao kutokuwa na uwezo wa kiuchumi wanashindwa kutimiza ndoto zao. Tangu tuanze mpango huu tumewarudisha shule na kuwapatia furaha waliyoikosa," anaongeza kusema.

Mmoja wa walionufaika na mradi huo, Kulthum Said, anasema haikuwa rahisi kwake kurudi shuleni kutokana na kukosa madaftari na sare, lakini Nyota Njema ilimsaidia mpaka sasa hivi anaendelea na masomo yake.

"Naishukuru Nyota Njema kwa kunisaidia kurudi shuleni, wazazi wangu waliniambia hawana uwezo wa kumudu kununua sare na madaftari nikabaki nyumbani kwa muda wa mwaka mmoja, lakini sasa naendelea na masomo yangu," anasema Kulthum.

Akizungumzia mradi wa mazingira, kiongozi huyo anasema kwamba kupitia 'mradi wa kijani' wanasaidia kuboresha mazingira kama upandaji wa miti, kusafisha maeneo mbalimbali ya wazi na utengenezaji wa bustani ya kupumzikia watu.

Anasema kwa kuanzia, wameomba kuboresha bustani ya Temeke Hospitali ili iwe na mvuto wa kipekee, hatua ambayo inaendelea kufanyika kwa kushirikisha Halmashauri husika.

Naye meneja mradi, Ibrahim Ally, ambaye alikuwa mwenyekiti wa kwanza wa kundi hilo, anasema waliangalia pia umuhimu wa watoto yatima kuwa na bima ya afya ili kuwarahisishia huduma za matibabu.

"Unajua idadi kubwa ya watoto yatima hawana uhakika wa kupata huduma za matibabu, mwaka jana tuliamua kuwakatia bima watoto 30 kwa kuanzia, mwaka huu tumepanga kuongeza idadi hiyo kama tukipata watu wa kutuunga mkono," anasisitiza.

Anasema wao kama vijana walioamua kujitolea, hawana fedha za kutosha, wanachokifanya ni kujichangisha kidogo walichonacho na kisha kutafuta ufadhili kwa watu na taasisi watakaoguswa na wazo lao.

"Ukweli hatuna fedha za kukamilisha miradi yetu yote, tunawashukuru baadhi ya taasisi na watu wanaotuunga mkono katika hiki tunachokifanya. Tunaomba watu watakaoguswa kutuunga mkono ili tuwafikie watu wengi ambao wanahitaji kurudisha matumaini," anasema Ally.



Mweka hazina wa Nyota Njema, Hemed Lumeme, akikabidhi msaada wa chakula kwa watoto yatima.

**"Naishukuru Nyota Njema kwa kunisaidia kurudi shuleni, wazazi wangu waliniambia hawana uwezo wa kumudu kununua sare na madaftari nikabaki nyumbani kwa muda wa mwaka mmoja, lakini sasa naendelea na masomo yangu,"**

HABARI KIMATAIFA

# Kenya kuwa jaribio chanjo ya corona

**LONDON,** Kenya

WANASAYANSI wanaotafiti chanjo ya corona kutoka Uingereza, wanafikiria kufanyia majaribio nchini Kenya.

Hatua hiyo inakuja baada ya wiki moja Shirika la Afya duniani, kuyaonya mataifa ya Ulaya kutolitumia bara la Afrika kama uwanja wa majaribio ya chanjo.

Mkuu wa Shirika hilo, Dk. Tedros Adhanom Ghebreyesus (pichani chini), alilaani kauli alizoziita za kibaguzi kutoka kwa madaktari wawili wa Ufaransa ambao walitaka chanjo ya virusi vya corona kufanyiwa majaribio Afrika.

Hata hivyo, wanasayansi hao kutoka Chuo kikuu cha Oxford, wanadaiwa kufikiria wazo hilo iwapo hawatapata matokeo ya haraka nchini Uingereza.

Chanjo hiyo inajulikana kutoa 'antibody' yenye nguvu, lakini hilo halimaanishi kwamba inaweza kuwa kinga.

''Tutalazimika kuhitaji chanjo nyingi zinazofanyiwa majaribio. hivyo tutahitaji dozi nyingi na tutarajie mjadala mkubwa kuhusu ni mataifa gani ama ni kundi lipi la watu linalohitaji chanjo hiyo kwanza?'' alisema mwandishi wa BBC wa maswala ya tiba Fergus Walsh.

Walsh alisema kuna umuhimu kuwa makini na ahadi zinazotolewa kutokana na kile alichokitaja kuwa hamu ya chanjo hiyo kufanya kazi.

Hatahivyo, kulingana na Walsh, kundi hilo la Oxford lina rekodi nzuri ya kipindi cha miaka 30 iliopita ambapo limefanikiwa kutengeneza chanjo zilizofanikiwa dhidi ya aina nyingine ya virusi vya corona kama vile MERS, ambayo imefanikiwa katika majaribio yaliofanyiwa katika miili ya binadamu.

Hatahivyo kuna maswali kuhusu uamuzi wa kufanya majaribio chanjo hiyo nchini Kenya, licha ya wagonjwa wachache wa virusi hivyo kuripotiwa nchini humo.





Bajaji inayofanana na kirusi cha corona, likiendeshwa na mfanyakazi wa jiji la Chennai katika kuhamasisha watu kukaa ndani ya nyumba zao kujikinga na ugonjwa wa COVID 19, jana. **PICHA: AFP**

# Trump apendekeza sindano za kemikali kutibu corona

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amekosolewa baada ya kupendekeza utafiti ufanyike kubaini ikiwa virusi vya corona vinaweza kutibiwa kwa kudunga binadamu sindano za kemikali za kuua vimelea vya virusi na bakteria.

Katika hotuba yake, Truamp pia ametaka wagonjwa watibiwe kwa mwanga wa kieletroniki, wazo lililopingwa na madaktari.

Kauli yake imeungwa mkono na ofisa wake mmoja, ambaye alisema kuwa mwangaza wa jua na kemikali za kuua vimelea unaua maambukizi.

Kemikali za kuua vimelea ni sumu na inaweza kuhatarisha maisha ya binadamu endapo itachomwa kwa sindano.

Kemi kali hizo pia zinaweza kuwa hatari kwa matumizi kuanzia ngozi, macho na mfumo wa kupumua.

Katika mkutano wa kikosi kazi cha kukabiliana na virusi vya corona cha Ikulu, siku ya Alhamisi, ofisa huyo aliwasilisha matokeo ya utafiti wa serikali ya Marekani ambayo ulionyesha kuwa virusi vya corona vinaonekana kudhoofika hata vinapopigwa na mwangaza wa jua au joto.

Utafiti huo pia ulionyesha kuwa kemikali ya blichi inaweza kuua virusi katika mate na ute wa mfumo wa kupumua katika kipindi cha dakika tano, huku pombe ikiua kwa haraka zaidi.

William Bryan, ambaye ni kaimu mkuu wa Idara ya Sayansi wa usalama wa ndani na teknolojia, katika wizara ya mambo ya ndani, aliainisha katika mkutano na waandishi wa habari juu ya matokeo ya utafiti huo.

**Kama daktari wa dawa , ninaweza kupendekeza kudunga sindano ya kemikali za usafi ndani ya mapafu au mionzi ya UV ndani ya mwili kutibu COVID-19. Usifuate ushauri wa matibabu kutoka kwa Trump.**

Rais Trum, alielezaa kuwa utafiti huo unapaswa kuchukuliwa kwa tahadhari, huku akipendekeza utafiti zaidi ufanyike kuhusu matumizi ya kemikali za kuua vimelea.

"Kwa mfano tukipiga mwili na mionzi ya kielekroniki au ikiwa tukiupiga mwili na mwanga wa nguvu," alisema Trump, huku akigeuka kumtazama dokta Deborah Birx, Mratibu wa Ikulu wa shughuli za kupambana na virusi vya corona.

"Halafu nikasema, je, mfano uingize mwangaza ndani ya mwili, ambao unaweza kuuingiza kupitia mwili au kwa njia fulani nyingine. Ninadhani ulisema utapima hilo pia.. Inafurahisha," aliendelea kusema kiongozi hiyo.

Alizidi kufafanua "Halafu ninaona kemikali ya kuua vimelea ikiviua kwa dakika moja. Dakika moja, kuna njia tunaweza kufanya kitu kama hicho au kusafisha ?

Huku akijinyooshea kidole kwenye kichwa chake, Trump aliendelea kusema: "Mimi sio daktari, lakini niko kama mtu ambaye anayeweza kukufanya ufikirie vizuri na kukuambia je, unafahamu nini ."

Alimgeukia tena Dk. Birx na kuuliza ikiwa alishawahi kusikia lolote kuhusu matumizi ya joto na mwanga kutibu virusi vya corona.

Hata hivyo, mapendekezo hayo, yamepokelewa tofauti na madaktari ambao wameonya wazo la kiongozi huyo kwani inaweza kusababisha matokeo mabaya.

Daktari bingwa wa maradhi ya mfumo wa kupumua, Vin Gupta, ameiambia BBC kuwa dhana hii ya kudunga au kuingiza aina yoyote ya kemikali ya usafi ndani ya mwili ni kutowajibika na ni ya hatari .

"Ni njia ya kawaida ambayo watu huitumia wakati wanapotaka kujiua," alisema daktari huyo.

Kashif Mahmood, daktari katika eneo la Charleston, West Virginia, alituma ujumbe wake wa twitter akisema "Kama daktari wa dawa , ninaweza kupendekeza kudunga sindano ya kemikali za usafi ndani ya mapafu au mionzi ya UV ndani ya mwili kutibu COVID-19. Usifuate ushauri wa matibabu kutoka kwa Trump."

John Balmes, mtaalamu wa tiba ya mfumo wa kupumua katika Hospitali kuu ya Zuckerberg San Francisco, alionya kuwa hata moshi wa blichi unaweza kusababisha matatizo mabaya ya kiafya.

Aliliambia gazeti la Bloomberg News kwamba kuvuta hewa ya kemikali ya chlorine inaweza kuwa ni jambo baya kwenye mapafu. Njia ya hewa na mapafu havikutengenezwa kupokea kemikali za kuua vimelea.

Awali Trump aliipigia debe dawa ya malaria ya hydroxycloroquine, akisema inaweza kuwa tiba ya virusi vya corona, ingawa wazo lake hilo hivi karibuni. **BBC**

# HADITHI


# Mauaji Harusini- 9

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri, anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**




HAPO ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

Shani, ambaye pamoja na umri mdogo akiwa ni msomi, kwa sababu alipelekwa shule za gharama kubwa, tena akiwa na umri mdogo, lakini tayari mazingira yalimfanya akue kabla ya umri wake.

Akiwa ni mtoto pekee alijua kuwa anakabiliwa jukumu la kurithi utajiri wa baba yake na kuuendesha ili uzidi kuendelea badala ya kushusha chini au kuua kabisa.Kwa bahati nzuri baba yake hakumtenga, bali alijua mali zote za baba yake na pia jinsi ya kuziendesha kwa sababu Patiyo hakutaka binti yake pekee apoteze muda mwingi kusomea vitu vingine, badala yake alimpeleka nje nchi kusomea biashara na utawala.

Hata hivyo pale msibani akili yake ilikuwa kama nusu mfu. Pamoja na yote yale, lakini hakutegemea baba yake kufa mapema kiasi kile, tena kwa aina ile ya kifo.

"Jikaze mama, ndiyo ukumbwa." Alisikika mama mmoja wa makamo akimbembeleza Shani msibani hapo.

Lakini cha ajabu na yeye alikuwa analia. Baada ya taratibu zote kukamilika. Nyimbo mbalimali za kwaya, risala za ndugu na jamaa, pamoja na serikali pia, huku Jeshi la Polisi pia ikiapa msibani hapo kuwasaka usiku na mchana wote waliohusika kwenye vifo hivyo, watu walianza kutawanyika kwenye Makaburi ya Kinondoni.

Sasa walibaki wana ndugu ambao nao walianza taratibu zao za kimila. Hii hufanyika sana kwa makabila mbalimbali ya Kiafrika. Mara nyingi taratibu za mazishi wa Kidini yakishamalizika, hubaki wanandugu nao ili wafanye taratibu au za kimila jinsi wanavyofanya baada ya ndugu yao kufariki. Na hii kila kabila lina aina yake ya mila yao jinsi wanavyofanya.

Kila lenye mwanzo halikosi mwisho. Patiyo na Grace wakawa wamelazwa kwenye nyumba zao za milele. Ndugu zao kila mmoja sasa aliondoka eneo la makaburi ili maisha mengine yaendelee.

Kwa tabu, Shani aliingizwa kwenye gari na shoga zake Hidaya na Matha ili kumrudisha nyumbani akaanze maisha mapya peke yake bila wazazi.

******************************

Simu ya mkononi iliita kwenye mfuko wa mmoja aliyekuwa kwenye kikao. "Jamani si tulisema kuwa simu zizimwe kwenye kikao hiki?" Alisikika mmoja wa watu hao, aliyeonekana ni mkubwa kuliko wenzake wote.

**Tumtafute mganga, tupate gharama kubwa, amroge, halafu tukae siku kibao na kusubiri ni lini ataanza kuwa chizi, halafu akianza ndiyo twende mahakamani. We hujui kuwa jamii yote inaweza kutufikiria kuwa sisi tumehusika na jambo hilo?**

Hakuna aliyejibu, wakabaki wanamuangalia. Hata ambaye simu yake ilikuwa ikiita kwenye mfuko wake naye hakujibu kitu. Alichofanya ni kuotoa mfukoni na kuangalia jina la anayepiga. Badala ya kupokea akakata. Kama vile haitoshi akaizima kabisa.

"Ni nani?" Aliuliza tena mkubwa wa kikao kile huku akiwa ametoa macho.

"Ni mke wangu mama Rehema." Alijibu ambaye simu yake ilikuwa ikiita.

"Nilisema tangu mwanzo. Hiki kikao ni cha siri na cha hatari. Hatutakiwi simu zote ziwe wazi kwa sababu ya usalama. Kuhusu askari polisi wala sina wasiwasi nao sana kwa sababu hapa tulipo hakuna anayetufuatilia wala kusikia mazungumzo yetu. Lakini hatari kubwa kwetu ni wake zetu. Hawa ndiyo sumu kwetu. Wanawake si wa kujua jambo hili, wala kufahamu sisi tunataka kufanya nini. Kuweni makini sana ndugu zangu tusije tukaishia jela." Aliunguruma mkuu wa kikao hicho.

"Samahani kaka nilijisahau. Niliona kama nimezima hivi, lakini kumbe sikuwa nimeangalia vizuri. Ilikuwa haijazimika." Alijitetea.

Chumba hicho kilikuwa ni moja katika vyumba vya jiko la hoteli ya zamani mitaa wa Magomeni Mikumi.

Kiliombwa kwa ajili ya kikao cha familia. Walioomba walitaka hapo kwa sababu waliona kuwa hakuna mtu ambaye atawafuatilia. Mmoja wa kati ya watu hao walikuwa na uhusiano mzuri na mwenye nyumba hiyo ambaye eneo hilo alikuwa analitengeneza ili aweke maduka na si hoteli tena.

Ndani ya chumba hicho kikubwa kulikuwa na watu wanne tu. Wote ni wanaume na ni ndugu wa baba na mama mmoja.

Wenyewe walikiita kikao hicho ni cha kifamilia. "Nilisema tangu mwanzo, kikao hiki ambacho hakihusishi mwanamke si wake zetu wala dada zetu wawili ni cha siri kwa sababu tunachotaka kukifanya wao wakijua tu, basi ni kwamba wote hata pingu zitatuhusu. Ndiyo maana nilitaka usiri sana. Wake zetu wasijue hata tuko wapi. Na dada zetu pia." Alisema na kuendelea kumtazama ndugu yake kwa hasira.

"Paul, usirudie tena kufanya kosa la kizembe kiasi hicho." Alikazia macho.

"Ndiyo kaka Jim." Alijibu.

"Ninachotaka kusema hapa ni kile ambacho tulidokezana wenyewe baada ya kikao kizima cha familia na baada ya wanafamilia wenzetu kuondoka. Ni kwamba marehemu ndugu yetu Patiyo ameacha mali nyingi sana. Ameacha malori, mabasi, majumba, mahoteli, kampuni kubwa tatu, pesa nyingi benki na magari ya kifahari.

Cha ajabu ni kwamba sheria inasema kuwa vyote hivyo ni mali ya binti yake Shani. Yaani sisi na akili zetu wakubwa wazima tukubali kweli Shani arithi mali zote za baba yake. Mtoto mdogo kama yule. Tena wa kike. Halafu achukue mali ya ndugu yetu tuliozaliwa tumbo moja sisi tubaki hivi hivi kweli, halafu tukubali?" Aliongea Jim aliyeonekana ndiyo mkubwa kuliko wenzake kwenye kikao hicho cha watu wanne.

"Ndiyo maana kaka tumekuja hapa. Tufanyaje ili mali hizo zije kwetu tugawane sisi ndugu zake tuliozaliwa naye tumbo moja?" Aliuliza mmoja wa wana ndugu.

"George, ndiyo maana tuko hapa. Tunataka kupata ufumbuzi. Kumbuka ni kwamba tulizaliwa saba, ndugu yetu Patiyo amefariki. Tumebaki sita, lakini dada zetu kwa sababu ni wanawake tumewatoa kwa sababu hawa wasingeweza kulinda siri ya kutaka sisi tuchukua mali, kwa hiyo tunakaochukua ni sisi wanne tu. Ndiyo maana nataka kila mmoja atoe wazo wake, halafu tulifanyie kazi mara moja." Jim alizidi kuwapa muongozo ndugu zake.

"Mimi nadhani twende mahakamani. Tutafute wakili mzuri ili Shani asiwe mrithi pekee wa mali za baba yake Patito. Ikumbukwe bado ni mdogo. Miaka 23, tena mtoto wa kike aendeshe na kuogelea utajiri wa mamilioni, haiwezekani." Paul alikoleza maongezi.

"Hata tufanye nini. Shani ndiye mrithi halali wa mali za marehemu baba yake. hakuna yoyote wa kutengua hilo. Hata twende kwenye Mahakama ya Dunia. Hata tukusanye mawakili wote ulimwenguni ni kazi bure tu. Ni kesi rahisi sana hii. Na kwenye kikao cha familia si ulimsikia Mwansasheria wa marehemu ndugu yetu Patiyo alivyosema?" Ilikuwa ni sauti ya mchangiaji mmoja ambaye ndiyo kwa mara ya kwanza naye anaongea na kutoa mchango wake.

"Ni sawa mdogo wangu Ben, ndiyo maana tuko hapa, tufanyeje ili tusipate?" Jim alirejesha swali kwa ndugu zake.

"Wala tusipepese macho hapa. Ili mali kisheria irudi kwetu ni lazima Shani asiwepo. Yeye ndiyo pingamizi pekee la kisheria kwetu. Patiyo angekuwa na watoto watatu wanne au zaidi tungesema warithi ni wengi. Lakini hapa jinsi ilivyo ni kwamba wazazi wa marehemu ambao ni wazazi wetu pia wamefariki. Marehemu amefariki huku mkewe pia akiwa ameshafariki siku nyingi. Hana watoto wengi ana mtoto mmoja tu. Kama hayupo huyu Shani, kisheria ni kwamba mali inarudi kwa ndugu wa baba na mama mmoja. Ni Shani pekee ndiye anayeleta uzito hapa." Ben alizidi kuwafafanulia wenzake jinsi sheria inavyofanya kazi yake.

"Sasa tunafanyaje?" Paul aliuliza wenzake.

"Hapa ni kwamba Shani asiwepo tu. Yeye ndiye kipingamizi kwetu." Jim alitoa ushauri wake.

"Aende wapi sasa." George aliuliza.

"Mimi naona tumuendee kwa mganga, amroge awe mwendawazimu. Nadhani hii pekee inaweza kutufanya tukusanye mali ya ndugu yetu irudi kwenye ukoo wake." Ben alisema akiwaangalia wenzake na tabasamu juu.

Kicheko kikali kilisikika kutoka kwa Jim, akisha akapanua kinywa chake.

"Ben, yaani wewe mdogo wangu msomi mzima unawaza mambo ya kishirikina!" Akatikisa kichwa kukataa mpango huo.

"Tumtafute mganga, tupate gharama kubwa, amroge, halafu tukae siku kibao na kusubiri ni lini ataanza kuwa chizi, halafu akianza ndiyo twende mahakamani. We hujui kuwa jamii yote inaweza kutufikiria kuwa sisi tumehusika na jambo hilo?" Ben alitoa hoja kukataa mpango huo na kutoa ushauri wake.

"Mimi nafikiria kitu kimoja tu cha kufanya. Auawe. Akiuawa hakutakuwa na kipingamizi tena. Mali itakuwa yetu sisi wanne na tutagawana sawa bin sawia.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KADI YA BAJAJI IMEPOTEA

**RHODA C.MABUMO** amepotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC 822 BFZ.** Aina yake **TVS KING.** Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha polisi taarifa ya polisi : **MOR/MOR/RB/329423/2020.**

115715902

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No. 21 of 2020**

**In the matter of the estate of the late FRANK GILIARD MUSHI Of Mnadani within Dodoma City**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by CHARLES FRANK MUSHI**

**GENERAL CITATION**

***(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)***

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 15th day of MAY, 2020.

**Dated at Dodoma this 24th day of APRIL, 2020.**

........................................
RESIDENT MAGISTRATE

15715802

*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la Nipashe*

*kila siku Tupigie 0782253676*




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# WERNER AJIANDAA KUTUA LIVERPOOL




**MUNICH,** Ujerumani

MSHAMBULIAJI wa RB Leipzig, Timo Werner, yupo tayari kusajiliwa na Liverpool kama watalipa pauni milioni 52 ambazo zipo kwenye kipengele cha mkataba wake endapo akitaka kuondoka, kabla ya Juni 15.

Lakini Liverpool, kama ilivyokuwa Januari, hawana mpango wa kufanya uhamisho wa Werner kabla ya kumalizika kwa kipengele hicho cha mkataba. Werner, ambaye kipengele hicho kiliwekwa kwenye mkataba wake wakati alipoongezewa hadi kipindi cha majira ya joto mwaka 2023, alieelezea kujivunia kwake kuwaniwa na vinara hao wa Ligi Kuu ya England, Februari, mwaka huu.

Raia huyo wa Ujerumani alikaribia kujiunga na Bayern Munich kipindi cha majira ya joto kilichopita kwa ada ya euro milioni 30 na vinara hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, bado wanamuwania kumsajili.

Werner pia amemsifia raia mwenzake wa Ujerumani, Jurgen Klopp kama "kocha bora duniani" na anaamini staili ya uchezaji ya Liverpool inamfiti yeye kutua pale Anfield.

Amefunga mabao 27 katika mashindano yote msimu huu kwa RB Leipzig, yakiwamo manne kuisaidia timu yake kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Nafikiri (Liverpool itaimarika) pale mbele, na ndio maana wanafikiria kuhusu Werner," alisema akinukuliwa na gazeti la Bild.

# PSG kumrudisha Benzema Ufaransa

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya PSG imebainisha kwamba ipo mbioni kumsajili Karim Benzema, kama Edinson Cavani atakwenda kule Newcastle United.

Kwa mujibu wa Sky Sport, tajiri anayetaka kuinunua Newcastle anamuwania Cavani ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Uruguay ili kuimarisha kikosi hicho.

Lakini PSG wameripotiwa kwamba watatupa ndoano yao kwa Benzema wanayeamini ni mtu sahihi wa kuziba nafasi yake.

Cavani anayemaliza mkataba wake, anaweza kuondoka bure klabuni hapo na tayari imedaiwa ameshaanza kujiandaa kuwa na maisha nje ya kikosi hicho cha kocha, Thomas Tuchel.

Kwa mujibu wa taarifa zaidi, PSG inamtazama Benzema kama mtu sahihi wa kwenda kuunda upatina na Neymar na Kylian Mbappe.

Straika huyo Mfaransa, mwenye umri wa miaka 32, ameendelea kuwa na kiwango bora kwa misimu ya karibuni, ambapo kwa msimu huu amefunga mabao 19 katika mechi 36 za mashindano yote pale Real Madrid na mkataba wake unamalizika mwaka 2022.






# Van Persie na mkataba Arsenal

**AMSTERDAM,** Uholanzi

NAHODHA wa zamani wa Arsenal, Robin Van Persie, amefichua siri ya kuachana na klabu hiyo na kutimkia Manchester United mwaka 2012.

Taarifa za awali zilieleza mshambuliaji huyo aliondoka Arsenal baada ya kushindwa kuafikiana na uongozi juu ya maslahi yake kwenye mkataba mpya, ambao alihitaji uwe na vipengele vya kusajiliwa, wachezaji wenye hadhi ya kuipa mataji timu hiyo.

Lakini Van Parsie ambaye ameshastaafu soka, amefichua siri na kueleza uvumi huo haukuwa kweli, kwani wakati huo alitamani kuendelea kuitumikia Arsenal.

Alisema taarifa zilizotolewa wakati ule zilikua kinyume chake, kwani viongozi wa Arsenal waligoma kumpatia mkataba mpya na ndio maana alifanya uamuzi wa kuondoka.

"Hadi leo hii hakuna yeyote anayejua ukweli," alisema Van Persie akinukuliwa na Sky Sport.

Aliongeza: "Sikuwa na maelewano na Mtendaji Mkuu, Ivan Gazdiz, na ndio maana niliamua kuondoka, suala la mimi kuweka masharti makubwa kwenye mkataba mpya halikuwapo na wao wakakataa kunipa mkataba mpya."

Van Persie alisajiliwa na Man United chini ya kocha Sir Alex Ferguson kwa dau la pauni milioni 24 na alitwaa taji la England katika msimu wake wa kwanza Ngao ya Jamii.

Hadi anaondoka Arsenal mwaka 2012, Van Parsie alikua amefunga mabao 96 katika michezo 194 aliyocheza, na kwa upande wa Man United alicheza michezo 86 na kufunga mabao 48.

## HABARI MICHEZO

# Zanetti: Martinez anafurahia Inter Milan

**MILAN,** Italia

MAKAMU Rais wa Inter Milan, Javier Zanetti, anaamini Lautaro Martinez (pichani) ana furaha katika klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Italia, Serie A, wakati huu ripoti zikimhusisha na mpango wa kuwaniwa na Barcelona.

Martinez ameripotiwa kuwa ndio kipaumbele cha kwanza kwa usajili wa mabingwa hao wa LaLiga ambao wanamuona kama mrithi wa muda mrefu wa mshambuliaji Luis Suarez.

Pia amekuwa akihusishwa na klabu za Real Madrid na Manchester City, baada ya kufunga mabao 16 katika mechi 31 alizocheza msimu huu kwenye mashindano yote kabla ya ligi kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Zanetti aliulizwa kuhusu Martinez wakati wa mahojiano 'mubashara' kwenye Instagram na mshambuliaji wa zamani wa Inter, Christian Vieri na alisema: "Nitakuwa mkweli. Wakati tulipomchukua yeye, tulijua kwamba alikuwa mmoja wa vijana wa Argentina wanaochikupia na wenye vipaji vya ukweli.

"Na sasa kwa kazi ya kocha (Antonio) Conte, katika umri wake wa miaka 22, anaweza kutupa vitu vingi. Kwa sasa, kwa kila kitu kinachotokea, hatufikirii kuhusu nini atafanya.

"Halafu tutaona, lakini sasa namuona yeye akiwa na furaha kubwa hapa Inter. Na pamoja na Lukaku."

Martinez aliondoka Racing Club kwenda Inter mwaka 2018 na haraka amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa washambuliaji wakali zaidi kwenye soka la Ulaya.





# HUDSON-ODOI AMTAKA SANCHO CHELSEA

**LONDON,** England

CALLUM Hudson-Odoi amesema "angependa" kucheza pamoja na nyota wa Borussia Dortmund na anayewaniwa na Manchester United, Jadon Sancho pale Chelsea.

Sancho ni mchezaji anayewaniwa zaidi kwa sasa baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga akiwa na Dortmund, huku wapinzani wa EPL, United na Chelsea wakiripotiwa kukimbizana kuwania saini ya mchezaji huyo wa kimataifa wa England.

United inaaminika kama ipo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumsajili Sancho, mbele ya Chelsea, lakini winga wa 'Blues', Hudson-Odoi angependa kumuona mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, kwenye dimba la Stamford Bridge.

"Tuhakikishe kwamba wote tunafanya vizuri, kwa uhakika kabisa anafanya vitu vya kuvutia na amekuwa na msimu bora kabisa kwake," alisema Hudson-Odoi wakati wa mahijiano mubashara na kwenye mtandano wa kijamii wa Instagram.

"Mara zote tulikuwa tunahakikisha kila mmoja yupo vizuri. Kwa uhakika kabisa ni mchezaji mkubwa, napenda kucheza na yeye - ni mchezaji mkubwa kucheza naye.

"Kwa England tumecheza wote wakati tukikua na bado tuna mawasiliano mazuri tu. "Nimecheza naye mara kadhaa kwenye mechi za vijana au kwa England, mahusiano bado yako pale pale na mara zote tumekuwa tunapenda kucheza pamoja.

"Namna tunavyocheza kwa pamoja tunajua kila mmoja yupo upande gani wa uwanja na tunapenda sana kucheza pamoja. "Sijui (kama atakuja). Bilashaka, ningependa sana kama angekuja Chelsea.

"Tumekuwa na upatina mzuri kwa kipindi chote, namna tunavyocheza kwa pamoja inavutia. Kama akija upatina wetu utakuwapo hapa."

# *Serie A kuendelea hadi Agosti 2- FIGC*

**ROME,** Italia


MSIMU wa 2019-20 wa Ligi Kuu ya Serie A, utaendelea hadi Agosti 2, shirikisho la soka la Italia, (FIGC), limetangaza.

Umoja wa Mashirikisho ya Soka Ulaya (Uefa), Alhamisi, ulisisitiza kwamba, ligi zote za Ulaya ambazo zimesimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona zinatakiwa kumaliza msimu, ingawa yametolewa maelekezo kwa zile ambazo hazitaweza kuendelea.

Kamati ya Utendaji ya Uefa ilipendekeza kwamba, mashindano ya Ulaya na ligi zake zinatakiwa kwenda sawa wakati zitakaporejea tena ili zimalizike kwa wakati mmoja. Na Rais wa FIGC, Gabriele Gravina amethibitisha kwamba, muda wa ziada utatolewa kwa klabu kwa ajili ya kumalizia kipindi cha msimu kilichobaki.

Amesema watakuwa na mkutano wa majadiliano na Chama cha Wanasoka wa Italia (AIC), kuhusu kuongeza muda wa kumalizika kwa mikataba ya wachezaji kutoka Juni 30, kwa sababu ya kuchelewa kumalizika kwa ligi.

Timu za Serie A zinamatumaini kurudi kwenye mazoezi Mei 4, wakati amri ya kutotoka ndani itakapokuwa imemalizika nchini Italia.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# OZIL NA AUZWE TU - MASHABIKI ARSENAL

## Kisa kukataa kukatwa mshahara janga la corona kama wachezaji wenzake...

**LONDON,** England

BAADHI ya mashabiki wa Arsenal, wameshauri kiungo wao, Mesut Ozil auzwe baada ya mchezaji huyo kutoka Ujerumani kuripotiwa kuwa miongoni mwa wachezaji watatu waliokataa kukatwa mishahara yao.

Mapema wiki iliyopita klabu ya Arsenal ilitangaza kwamba, wachezaji wake wamekubali kukatwa mishahara yao kwa asilimia 12.5 ili kuweza kuwanusuru wafanyakazi wengine ndani ya klabu hiyo.

Hiyo ikiwa pia njia ya kulinda uchumi wa klabu kutokana na janga la virusi vya corona, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

**Hata hivyo, Ozil ni mmoja wa wachezaji ambao walikataa kukatwa mshahara wake kwa sababu hiyo.**

Ozil analipwa mshahara mkubwa zaidi kuliko mchezaji yeyote ndani ya Arsenal akiwa anapokea pauni 350,000 kwa wiki.

Hivyo, kukataa kwake kukatwa asilimia 12.5 ni jambo ambalo baadhi ya mashabiki wa klabu hiyo wamelipokea kwa hisia tofauti, huku wengine wakishauri ni bora auzwe.

Wachezaji wengine waliokataa kukatwa asilimia 12.5 ya mshahara wao hawajatajwa ingawa suala hili si la kimkataba, bali ni uamuzi wa mtu binafsi.

## ZISIKUPITE

### MARI KUFUNGWA ARSENAL

ARSENAL inapanga kukamilisa usajili wa kudumu kwa mlinzi wa Flamengo raia wa Hispania, Pablo Mari mwenye umri wa miaka 26, ambaye alijiunga na 'Washikabunduki' hao kwa mkopo Januari. ***(Athletic)***

### WILLIAN KUIBUKIA LIVERPOOL

KIUNGO wa Chelsea, Willian raia wa Brazil mwenye umri wa miaka 31, yuko kwenye mazungumzo ya kujiunga na Liverpool mara tu mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Mirror)***

### UNITED KUIUZIA PSG BEKI

KLABU ya Manchester United inafikiria kumuuza mlinzi wake kinda Diogo Dalot mwenye umri wa miaka 21, kwenda Paris St-Germain. ***(Daily Mercato)***

### YAMKOMALIA SANCHO

BORUSSIA Dortmund wako tayari kumfanya Jadon Sancho kuwa mchezaji wao wa pili anayelipwa fedha nyingi zaidi ili aendelee kubaki kwenye klabu hiyo, licha ya kutolewa macho na Manchester United na Chelsea. ***(Forbes)***

### COUTINHO APELEKWA CHELSEA

PILIPPE Coutinho anaweza kurudi kwenye ubora wake kama kiungo huyo mwenye umri wa miaka 27, raia wa Brazil ataondoka Barcelona na kujiunga na Chelsea, kwa mujibu wa gwiji wa Brazil, Rivaldo. ***(The Sun)***

### WERNER TAYARI KUTUA LIVER

MSHAMBULIAJI wa RB Leipzig, Timo Werner, mwenye umri wa miaka 24, yuko tayari kujiunga na Liverpool iwapo italipa pauni milioni 52 iliyopo kwenye kipengele cha kuvunja mkataba wake kabla ya Juni 15. ***(Sky Sports)***

### LEICESTER YAJITOSA KWA PEA

KLABU ya Leicester City inajiandaa kuikabili Manchester United kwenye mbio za kuwania kumsajili mshambuliaji wa Borussia, Monchengladbach na Ufaransa, Alassane Pea, mwenye umri wa miaka 27. ***(Le10 Sport)***

### JUVE KWA STRAIKA WA NAPOLI

MIAMBA wa soka la Italia, Juventus, wanaangalia uwezekano wa kutoa ofa wakati wa kipindi cha majira ya joto kwa klabu ya Napoli ili kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Poland, Arkadiusz Milik mwenye umri wa miaka 26. ***(Calcio Mercato)***

### ATERTA AMULIKA FEYENOORD

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, anataka kumsajili kiungo wa Feyenoord, Orkun Kokcu, mwenye umri wa miaka 19, huku miamba hao wa Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, wakitaka kuuza wachezaji wake ili kusajili wanaowahitaji zaidi wakati wa majira ya joto. ***(Voetbal International)***

### MKHITARYAN ANOGEWA ITALIA

KIUNGO wa Arsenal raia wa Armenia, Henrikh Mkhitaryan, mwenye umri wa miaka 31, ana matumaini ya kubakia nchini Italia katika klabu ya AS Roma msimu ujao baada ya kucheza hao kwa mkopo. ***(Athletic)***

### ROMA KUMBAKISHA SMALLING

KLABU ya AS Roma imepanga kumsajili moja kwa moja mlinzi wa Manchester United, Chris Smalling, 30, anayechezea timu hiyo ya Serie A kwa mkopo. ***(Daily Mail)***

## HABARI MICHEZO

# CHIRWA AFUNGWA AZAM FC NGOMA AKIMSIKILIZIA KOCHA

**Na Saada Akida**

WAKATI Azam FC ikimuongeza Obrey Chirwa mkataba wa mwaka mmoja, ambao utamwezesha kusalia katika dimba la Chamazi hadi 2021, uongozi wa klabu hiyo, umesema hatma ya mshambuliaji Donald Ngoma kuendelea na kikosi hicho kwa msimu ujao ipo mikononi mwa kocha Mromania Aristica Cioaba.

Mkataba wa awali wa Chirwa ambao aliongeza Juni mwaka jana, ulikuwa unamalizika mwishoni mwa msimu huu, hivyo kwa kusaini tena kutamfanya aendelee kusalia dimba la Chamazi hadi mwishoni mwa msimu ujao.

**Mara baada ya kusaini mkataba huo jana, mbele ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat', Chirwa alisema: "Nawaomba mashabiki huu mwaka kwangu nishafanya vizuri, nitaendelea kufanya vizuri na mwaka huu 2020 nitaendelea kuwafurahisha mashabiki wa Azam, nawaomba tu uwanjani waje kwa wingi."**

Aidha, akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Popat, alisema mkataba wa Ngoma unamalizika Julai mwaka huu, na wanachosubiri ni mapendekezo kutoka benchi la ufundi.

Alisema hawajaanza mazungumzo na mchezaji huyo, kwa sababu ya kutopata taarifa kutoka kwa kocha wao pia nyota huyo yupo kwao Zimbabwe katika mapumziko haya yaliyosababishwa na mlipuko wa virusi vya corona.

"Ngoma bado ni mchezaji wetu, mkataba wake unaisha mwezi wa saba mwaka huu, sasa tunasubiri kocha akisema mchezaji huyo yupo katika mipango yake ya msimu ujao tutamuongeza mkataba.

"Tunasajili kulingana na mapendekezo ya benchi la ufundi, hivyo tumewaongezea baadhi ya nyota wetu ikiwamo Chirwa na wengine," alisema Popat.



Mshambuliaji wa Azam FC, Obrey Chirwa (kushoto), akisaini mkataba mpya mbele ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat', jana, jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mbeya City yataja ilipojikwaa Ligi Kuu Bara

**Na Saada Akida**

KATIBU Mkuu wa Mbeya City, Emmanuel Kimbe, amesema mabadiliko ya benchi la ufundi yamekuwa chanzo kikubwa kwa timu yao kusuasua katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kimbe alisema msimu huu hawakuwa vizuri kutokana na kuanza vibaya ligi hiyo kwa sababu ya mabadiliko makubwa katika benchi la ufundi na wachezaji wengi kuondoka.

Alisema kuondoka kwa wachezaji wao wengi katika kikosi cha kwanza kuliwaletea shinda kwa kuanza kukijenga upya.

"Msimu huu tumeanza kwa kusuasua, hatutafuti mchawi, tumegundua kwamba tatizo ni mwenendo wa timu yetu wa kufanya mabadiliko ya benchi la ufundi huku kila kocha akija na mfumo wake," alisema Kimbe.

Alisema msimu huu hawajatulia na kikosi chao hakijaonesha kile ambacho kilikuwa kikitarajiwa na mashabiki wa soka na mashabiki wa timu hiyo.

Mbeya City ipo katika nafasi ya 17 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 30 baada ya kushuka dimbani mara 29.

# Ligi Kuu yampasua kichwa Hererimana

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa KMC, Haruna Hererimana, amesema anaumiza kichwa ni kwa namna gani timu hiyo itafanya vizuri katika mechi ngumu zilizobaki ili kujihakikishia nafasi ya kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

Hadi Ligi Kuu inasimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, KMC FC, ipo nafasi ya 15 ikiwa na pointi 33 zilizotokana na mechi 29, ambazo si salama sana kuweza kujihakikishia kubaki katika ligi hiyo msimu ujao.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Kocha huyo alisema wako katika nafasi inayowahakikishia kubaki, lakini bado wanamechi ngumu kuliko za awali.

Alisema kwa nafasi waliyopo katika msimamo si mbaya, ila ushindani mkubwa kwa timu za chini ambazo wanajinasua kushuka inafanya ligi hiyo kuwa ngumu kwao.

"Bado tunahitaji kupambana, kufanya vizuri katika michezo iliyobaki nafasi tuliyokuwapo haitatufanya tukabweteka na kujiaminisha ligi bado ni ngumu," alisema kocha huyo.

Alisema sasa anahimiza wachezaji wake kuzingatia mazoezi ili wanaporejea katika ligi wawe fiti kusaka pointi katika michezo iliyobaki.



# *Nahodha Yanga aota 'mavitu' ya Morrison*

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU majaliwa ya kurejea kwa Ligi Kuu yakiwa bado hayajajulikana, nahodha msaidizi wa Yanga, Juma Abdul, ameendelea kuota manjonjo ya mshambuliaji wao, Mghana Bernard Morrison.

Ligi Kuu imesimama kwa kipindi kisichojulikana kutokana na mlipuko wa virusi vya corona ambavyo vinaitesa dunia kwa sasa kutokana na watu wengi kupoteza maisha duniani kote.

Morrison (pichani) ambaye alisajiliwa katika dirisha dogo la msimu huu, amekuwa kivutio si tu kwa wachezaji wenzake bali mashabiki wa timu hiyo pia, huku watani zao Simba wakimkumbuka baada ya kuifunga bao pekee lililowalaza na 'viatu' mapema wakati wakichezea kichapo cha goli 1-0 kwenye mzunguko wa pili wa Ligi Kuu.

Na kutokana na wachezaji wote kuendelea na mazoezi binafsi, Abdul amesema kwa sasa wamekuwa wanyonge nyumbani kutokana na kushindwa kuendelea kupambana kwenye Ligi Kuu Bara.

"Mambo ni mengi ambayo nimekumbuka ndani ya ligi ikiwa ni pamoja na vitu vya Morrison uwanjani ukiachana na hayo pia namna ambavyo mashabiki walikuwa wanatupa sapoti ilikuwa ni raha.

"Kwa sasa muda mwingi ninautumia nikiwa nyumbani na mazoezi ninafanya bila uwapo wa kocha, ni balaa tupu yaani ninapenda hali irejee kama zamani maisha yaendelee," alisema Abdul.

# Michezo

Jumamosi Aprili 25, 2020

Nipashe




Ozil na auzwe tu - Mashabiki Arsenal

UKURASA 22

## SONSO APATA JIKO...



Beki wa Yanga SC, Ally Abdulkarim Mtoni 'Sonso' (kushoto), akiwa na mkewe baada ya kufunga ndoa Mbagala jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni mpambe wa Sonso, kiungo wa Simba, Said Hamisi Ndemla. **Na MPIGAPICHA**

## Werner ajiandaa kutua Liverpool

**MUNICH,** Ujerumani

MSHAMBULIAJI wa RB Leipzig, Timo Werner, yupo tayari kusajiliwa na...



HABARI UK.20

## Hudson-Odoi amlilia Sancho Chelsea

**LONDON,** England

CALLUM Hudson-Odoi amesema "ange-penda" kucheza pamoja na nyota wa...



HABARI UK. 21

# MAMILIONI YA MO YAMSUBIRI KAGERE

## Wakala afunguka huku APR ikimkana, mashabiki Simba washushwa presha baada...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kuhusishwa na timu nyingi kutaka kumsajili kinara wa mabao Ligi Kuu Bara, Mnyarwanda Meddie Kagere, ambaye mkataba wake na Simba unaelezwa kumalizika msimu huu, wakala wa mshambuliaji huyo, Patrick Gakumba amewatuliza mashabiki wa timu hiyo baada ya kueleza kilichobaki ni kufuata mamilioni ya Mwekezaji wa klabu hiyo, Mohamed 'Mo' Dewji.

**Mshindi huyo wa Kiatu cha Dhahabu Ligi Kuu Bara msimu uliopita, hadi ligi hiyo inasimama msimu huu yupo kileleni mwa orodha ya wafungaji akiwa na mabao 19 wakati huu Simba ikiwa imebakiza mechi 10 kabla ya ligi kumalizika.**

Hata hivyo, licha ya kuwa kwao kwa mapumziko kutokana na Ligi Kuu kusimama kwa sababu ya mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19, Kagere amehusishwa na klabu nyingi ikiwamo APR ya nyumbani kwao, lakini wakala wake amekana ikiwa ni pamoja na uongozi wa klabu hiyo ya Rwanda.

Awali Rais wa APR, Jack Musemakweli, alidaiwa kufanya mazungumzo na wakala wa Kagere, lakini msemaji wa klabu hiyo, Clever Kazungu, alimwambia mwandishi wetu kuwa taarifa hizo si za kweli na kama ingekuwa hivyo wangebisha kwanza hodi kwa uongozi wa Simba.

"Tunajua taratibu za kufanya kwa mchezaji tunayehitaji kumsajili, halafu klabu yetu [APR], kazi yetu ni kuzalisha wachezaji na kuwauza na ndiyo maana tuna akademi ya vijana hapa, Kagere si mchezaji wa kurudi klabu za Rwanda labda apate nyingine kubwa zaidi ya Simba nje ya nchi," alisema Kazungu.

Kazungu aliongeza: "Hizi taarifa si nzuri kwani zinaleta mshtuko hata kwa Kagere ambaye yupo mapumzikoni na familia yake, tunajua ataendelea kubaki Simba na kuifungia mabao hata 30 msimu huu."

Hata hivyo, kabla ya hapo wakala wa Kagere, Gakumba alishusha kabisa presha ya mashabiki wa Simba baada ya awali kueleza kuwa ni kweli mkataba wa Kagere unamalizika, lakini tayari wameshafikia mazungumzo na Mo na kwamba kilichobaki ni wao kuja kuchota mamilioni kutoka kwa tajiri huyo.

"Ni kweli mkataba wa Kagere unamalizika, lakini tumeshafanya mazungumzo na kukubaliana na kilichobaki ni kuja kuchukua mamilioni kutoka kwa Mo, kinachotuzuia ni kutokana na mipaka ya nchi kufungwa baada ya kuibuka mlipuko wa virusi vya corona," alisema.

Gakumba alisema Mo hawezi kushindwa kumbakisha mchezaji huyo anayeongoza kwa mabao Ligi Kuu na kwamba kila kitu wameshakubaliana.

Simba imebakiza ponti 11 tu katika mechi 10 zilizobaki ili kutangazwa bingwa wa Ligi Kuu Bara kwa msimu wa tatu mfululizo, baada ya kuvuna alama 71 katika mechi 28 ilizocheza na kuiwezesha kukaa kileleni mwa ligi hiyo ikifuatiwa na Azam FC yenye alama 54 na Yanga pointi 51, lakini watani zao hao wakiwa nyuma mchezo mmoja.

Kama Simba itatwaa tena ubingwa huo utaiwezesha kwa mara ya tatu mfululizo kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya msimu huu kutolewa mapema na UD Songo ya Msumbiji licha ya msimu uliopita kufika hatua ya robo fainali.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042